**Kimbunga** Jobo chayeyuka, TMA yatoa ufafanuzi

UKURASA 3



**Rais** Mwinyi awapa mwongozo wa kazi makamanda wapya

UKURASA 17



**Salah ajiwekea rekodi Liver**

UKURASA 21

Jumatatu Aprili 26, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580562

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Maagizo saba kuleta neema mafao NSSF

UKURASA 2



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**DK. MPANGO KUONGOZA KONGAMANO MUUNGANO**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, anatarajia kuwa mgeni rasmi katika...

UKURASA WA 4

**RC ASIMULIA ALIVYOPAMBANA KUMFUNGA MBAKAJI SHINYANGA**

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amesimulia kesi ya ubakaji...

## Wakimbia na mabilioni ya Bodi Mikopo Elimu Juu

UKURASA 2

## Wakurugenzi wa Temeke, Sumbawanga wasimamishwa

UKURASA 3

**MICHEZO** **PRISONS YAITANGAZIA VITA YANGA** UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mpango kuongoza kongamano Muungano

Na Christina Mwakangale

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, anatarajia kuwa mgeni rasmi katika kongamano la kuadhimisha miaka 57 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar leo.

Kwa mujibu wa Idara ya Habari (MAELEZO), kongamano hilo linatarajiwa kufanyika jijini Dodoma kuanzia asubuhi.

Sherehe hizo huadhimishwa kila mwaka kwa matukio tofauti ikiwamo gwaride maalum huku zikitumika pia kwa Rais kutoa msamaha kwa wafungwa.

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulifanyika Aprili 26 mwaka 1964 kukizaliwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mkataba wa Muungano huo ulitiwa saini Aprili 22 mwaka 1964 na aliyekuwa Rais wa Tanganyika kipindi hicho, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Hayati Shehe Abeid Amani Karume kisiwani Zanzibar.

Kanuni za msingi za Muungano wa mwaka 1964 zinaeleza kwamba chimbuko la Muungano pamoja na mambo mengine, linajumuisha uhusiano wa karibu wa muda mrefu kati ya watu wa Tanganyika na Zanzibar.

Uhusiano huo ni unagusa mambo mengi yakiwamo kisiasa yaliyotokana na harakati za kupigania uhuru na imani ya pamoja ya uhuru wa Afrika yote. Muungano huo unatajwa kuwa wa kwanza kwenye Bara la Afrika kutokana na kuungana kwa mataifa mawili huru, yanayojitawala.

# Serikali yatoa maagizo 7 NSSF kuondoa kero kwa wanachama

Na Mwandishi Wetu

KATIKA kuhakikisha changamoto zinazowakabili wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) zinatatuliwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, ametoa maagizo saba kwa mameneja wa mikoa yote ya NSSF ambayo yatakuwa mwarobaini wa kumaliza changamoto hizo na kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Waziri Jenista alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, katika kikao kazi alichokiitisha na Mameneja wa Mikoa yote ya NSSF, maofisa wasimamizi wa wilaya, wasimamizi wa vituo vidogo na maofisa utekelezaji nchi mzima.

Moja ya maagizo hayo kwa watendaji wa Mfuko huo ni kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia dira na dhima ya NSSF katika kutoa huduma na kuondoa kero za wanachama na wadau wao.

"Kila mmoja wetu akiondoka hapa akatimize wajibu wake hasa katika kupunguza ama kumaliza zile changamoto zinazowakabili wanachama ili tuweze kufikia malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Mama Samia, ya kutatua kero mbalimbali zilizopo katika sekta ya hifadhi ya jamii," alisema. Kwa mujibu wa Waziri Jenista, Mfuko huo unatekeleza majukumu manne ya msingi ikiwamo kuandikisha wanachama kutoka sekta rasmi na sekta isiyo rasmi, kukusanya michango, kuwekeza na kulipa mafao kwa wanachama.

Agizo la pili ni kufanyika ukaguzi wa mara kwa mara kwa waajiri wote, kutokana na kubainika kwa uzembe katika eneo hilo unaofanywa na baadhi ya watumishi wa Mfuko, na kwamba wizara yake itafanya ziara za kushtukiza na ikiwezekana itahusisha vyombo vingine katika kuwafuatilia watendaji wa mikoani na wanaojihusisha na rushwa.

Katika agizo la tatu, Waziri Jenister aliwataka watendaji kusimamia sheria na miongozo mbalimbali inayolinda maslahi ya wafanyakazi pamoja na kusimamia vizuri utaratibu wa kulipa mafao ili kupunguza malalamiko.

Waziri Jenista katika agizo lake la nne aliwaagiza wafanyakazi wa Mfuko huo kuzingatia utoaji wa huduma bora kwa wanachama ikiwa ni pamoja na kujenga utamaduni wa ufuatiliaji na kutopuuza malalamiko ya wanachama.

La tano; aliwataka kupima utendaji kazi wao ili kufikia malengo na kufanya mapitio ya mpango mkakati ili kuona uhalisia wa malengo waliojiwekea ikiwamo kuwa waadilifu na wazalendo kwa Mfuko na kuzingatia maadili ya utumishi.

Agizo la sita; ni watendaji wa Mfuko huo kuendelea kutatua changamoto mbalimbali katika utoaji huduma kwa wanachama kwa kuwa bado kuna changamoto ambazo Mfuko unatakiwa kuzifanyia kazi ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Katika agizo lake la mwisho; Waziri Jenista aliwaelekeza watendaji wa Mfuko huo kuja na mkakati wa uhamasishaji na utoaji elimu ili kuandikisha wanachama wengi kutoka sekta isiyo rasmi.

Naye, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi), Profesa Jamal Katundu, aliwataka watendaji wa Mfuko huo kutekeleza malengo yote waliyoyaahidi na kuwataka wafanyakazi kufanyakazi kama timu moja, kuongeza ubunifu na kutoa huduma bora kwa wanachama. Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, alisema Mfuko utaendelea kuboresha huduma ili kukidhi matarajio ya wanachama pamoja na kutimiza malengo na maagizo ya serikali yaliyotolewa na Rais Samia kuhusu Hifadhi ya Jamii kuwa karibu na sekta binafsi.

Alisema ili kuboresha utendaji, Mfuko unaendelea kufanya mapitio ya mifumo yote ikiwamo sera na miongozo mbalimbali ili uweze kutimiza malengo yakiwamo ya kuandikisha wanachama, kukusanya michango, kuwekeza na kulipa mafao bora.



Mkuu wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, akimtwisha ndoo ya maji mmoja wa wanaume baada ya kuzindua kituo cha kutochea maji kwenye mradi ambao unatarajia kunufaisha zaidi ya wakazi 3,000 wa Kata ya Litisha wilayani Songea mwishoni mwa wiki. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

# Wakimbia na mabilioni ya Bodi Mikopo Elimu ya Juu

Na Sanula Athanas, DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), amebaini dosari katika ukusanyaji wa madeni ya wanufaika wa mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2019/20 iliyowasilishwa bungeni hivi karibuni, CAG Charles Kichere, anabainisha kuwa hadi kufikia mwaka wa fedha 2016/17, kulikuwa na ongezeko la wadaiwa sugu wa mikopo wapatao 128,278 kutoka 112,922 wa mwaka 2015/16.

Hata hivyo, taarifa zilizotolewa na HESLB, zilionyesha kuwa kulikuwa na wadaiwa sugu wa mikopo wapato 18 pekee, huku bodi hiyo inategemea fedha kutoka serikalini kwa karibu theluthi mbili ya bajeti yake.

Anasema ripoti ya usimamizi wa ulipaji na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu ilibainisha bodi haikuwa na ufanisi katika mifumo ya kuhakikisha kuwa inakusanya fedha kupitia ulipaji na urejeshaji wa mikopo ili kupunguza utegemezi kwa serikali kuu.

"Katika kipindi cha miaka mitano, bodi imekusanya asilimia 40 tu (shilingi bilioni 199) kati ya Sh. bilioni 492.

"Halikadhalika, ripoti ilionyesha udhaifu wa urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika wadaiwa. Ripoti imeonyesha kuwa, kulikuwa na jumla ya wanufaika wa mkopo 112,922 wanaodaiwa Sh. bilioni 706.7. Yote haya yalichangia utegemezi mkubwa wa bodi kwa serikali," anasema.

CAG anasema sababu zilizobainika za ulipaji na urejeshaji usioridhisha wa mikopo zinajumuisha kushindwa kutafuta idadi ya kutosha ya wanufaika wa mikopo, bodi ikishindwa kufuatilia angalau nusu ya mikopo inayostahili kulipya katika kipindi cha miaka minne.

Anasema sababu nyingine ni bodi kushindwa kuhakikisha wanufaika wa mikopo wanalipa mikopo kikamilifu, akibainisha kuwapo kwa mikopo inayostahili kulipwa inayofikia Sh. bilioni saba katika kipindi cha zaidi ya miaka mitano.

CAG anaitaja sababu ya tatu kuwa ni njia duni za ukusanyaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika wadaiwa waliopatikana.

"Ilibainika kuwa bodi ilikusanya Sh. bilioni 221 tu kati ya Sh. trilioni 2.4 kutoka kwa wadaiwa waliopatikana kwa miaka mitano ya fedha kuanzia mwaka 2012/13 hadi 2016/17.

"Upatikanaji endelevu wa rasilimali kwa wanufaika wapya wa mikopo uko hatarini kwani bodi haitakuwa na fedha za kutosha kuwakopesha wanafunzi wapya wanaostahili.

"Utegemezi wa bajeti ya nyongeza kutoka serikali kuu kwa utendaji na shughuli endelevu za bodi utaendelea," CAG abatahadharisha.

Anabainisha kuwa kanzidata ya HESLB ilihifadhi jumla ya wanufaika wa mkopo 112,922 ambao walikuwa na madeni ya mikopo ya jumla ya Sh. bilioni 706.7 na hawakurejesha kwa zaidi ya miaka mitano (hadi 2015/16).

"Kwa mujibu wa Mwongozo wa Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo wa Mwaka 2008, wanufaika hawa wa-

## HABARI KITAIFA




Wanafunzi wa Shule za St Mary's wakiimba katika hafla ya Kusherehea Maisha ya Utumishi wa Hayati Dk Askofu Getrude Lwakatare wa Kanisa la Mlima wa Moto Mikocheni jijini Dar es Salaam zilizofanyika jana. Askofu Dk Lwakatare alifariki mwaka jana na kuzikwa kwenye eneo la kanisa hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakurugenzi wasimamishwa

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu, amewasimamisha kazi wakurugenzi wawili wa mamlaka za serikali za mitaa ili kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili.

Taarifa iliyotolewa na wizara hiyo jana kwa vyombo vya habari, ilibainisha waliosimamishwa ni pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, Nyangi Msemakweli, ambaye anakabiliwa na tuhuma za ubadhirifu, usimamizi mbovu wa miradi ya maendeleo, uhusiano usioridhisha ná madiwani, Mkuu wa Wilaya na viongozi wengine wa wilaya na Mkoa wa Rukwa.

Mwingine aliyekumbwa na rungu hilo ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Lusubilo Mwakabibi, baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi, viongozi na vyanzo vingine kuhusu tuhuma za mwenendo usiofaa, matumizi mabaya ya madaraka, ubadhirifu na usimamizi usioridhisha wa miradi ya maendeleo katika Manispaa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, baada ya kuwasimamisha kazi wakurugenzi hao, Ummy alimwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI, kutuma mara moja timu ya watalaamu kwa ajili ya kufanya uchunguzi.

Waziri Ummy pia aliwaelekeza wakuu wa mikoa yote kusimamia vyema shughuli za maendeleo na kutekeleza miradi katika mikoa yao.

Pia, aliwaagiza wakurugenzi na watendaji wote kwenye halmashauri, kuheshimu mipaka yao ya kazi na kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu.

Ummy alisema serikali haitasita kuwachukulia hatua za kisheria na kinidhamu watumishi watakaobainika na ubadhirifu na kukiuka sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Hivi karibuni, Mwakabibi alituhumiwa kuwaagiza askari polisi kuwashikilia baadhi ya waandishi wa habari waliokuwa wanatekeleza majukumu yao katika Manispaa ya Temeke.

Pia, baadhi ya tuhuma zinazomkabili Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Sumbawanga, ziliwasilishwa bungeni jijini Dodoma na mmoja wa wabunge, aliyedai kiongozi huyo haelewani na baadhi ya watendaji wilayani huko.

# Viwanja 400 wadaiwa sugu kupigwa mnada

**Na Rose Jacob,** MWANZA

ZAIDI ya viwanja 400 vya wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi, vinatarajiwa kuuzwa kwa mnada kutokana na kushindwa kulipa madeni kwa mjibu wa sheria.

Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa Mkoa wa Mwanza, Elia Kamihanda, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki jijini hapo kuwa watu hao wanadaiwa Shilingi bilioni tatu.

Akizungumza na gazeti hili, Kamihanda alisema viwanja 421 vipo Wilaya za Ilemela, Nyamagana na Magu.

"Uuzaji wa viwanja hivi umetokana na mahakama kuwapatia wadaiwa hao sugu siku 14 wawe wameshalipa madeni yao ya kodi ya ardhi, lakini wameshindwa kufanya hivyo na mahakama kumpatia idhini dalali Rock City Takers kuviuza," alisema.

Wadaiwa hao sugu ambao viwanja vyao vitapigwa mnada walikuwa hawajalipa kodi hiyo kuanzia kipindi cha miaka mitano hadi 10 na katika idadi ya 736 waliolipa ni 315 kiasi cha Sh. milioni 900.

Kwa mjibu wa Sheria ya Ardhi, kama mmliki akipokea hati ya kumtaka kulipia deni lake ndani ya siku 14 na akishindwa, Kamishna wa Ardhi amepewa haki ya kumfikisha mahakamani mdaiwa ndani ya siku siku 14.

# Kimbunga jobo kilivyoyeyuka

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA) imesema kimbunga Jobo kilichokuwa kinatarajiwa kuikumba Tanzania, kimeyeyuka.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mamlaka hiyo jana, kimbunga hicho kilitarajiwa kuingia nchini kuanzia Aprili 24 na kuleta madhara, hasa kwenye mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara pamoja na visiwa vya Mafia na Zanzibar.

Maeneo mengine yaliyotarajiwa kuathirika kutokana ná kimbunga hicho ni ya kanda ya ziwa kutokana na mkandamizo wa hewa ambao ulitarajiwa kuvuta unyevunyevu katika misitu ya Kongo na kusababisha mvua kubwa nchini.

"Mwenendo wa kimbunga unaonyesha kuwa katika kipindi cha saa sita zilizopita, Jobo imepoteza nguvu yake wakati kimbunga hicho kikiingia nchi kavu kusini mwa Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam usiku wa Aprili 24 mwaka huu," TMA ilibainisha katika taarifa yake ya jana na kutoa ufafanuzi zaidi kwamba:

"Hali hii ilisababishwa na kuendelea kuimarika kwa upepo kinzani katika mwelekeo wa kimbunga hicho. Vilevile, mawingu ya mvua yaliyokuwa yakiambatana na kimbunga hicho yamesambaa baharini karibu na maeneo ya kusini mwa pwani ya Tanzania na Msumbiji.

"Hivyo kwa sasa, kimbunga hafifu 'Jobo' hakipo katika nchi yetu na hakuna madhara ya moja kwa moja yanayotarajiwa. Hata hivyo, masalia ya mawingu yanayoambatana na kilichokuwa kimbunga 'Jobo' yanaweza kusababisha mvua katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani."

TMA iliwashauri wananchi kuendelea kufuatilia na kuzingatia taarifa za utabiri kutoka kwa mamlaka hiyo pamoja na maelekezo na miongozo inayotolewa na mamlaka husika.

Awali, kimbunga hicho ambacho kilitarajiwa kuwa na upepo mkali, kilikuwa na kasi ya kilomita 60 kwa saa lakini kadri kilivyokuwa kikisogea na kukutana na hali ya hewa kinzani, kasi yake ilizidi kupungua.

Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk Agnes Kijazi, akizungumzia historia ya kimbunga hicho mbele ya waandishi wa habari juzi, alisema si kawaida kutokea kwa vimbunga nchini.

"Nchi yetu ipo karibu sana na Ikweta, mara nyingi vimbunga hivi vinatokea kusini zaidi ya Ikweta, hiki kinachotarajiwa kufika hapa kwetu kwa mara ya mwisho kilitokea Dar es Salaam mwaka 1872 lakini pia kiliwahi kutokea Lindi mwaka 1952, hivyo ukiangalia ni nadra sana kutokea kimbunga hapa kwetu.

"Vimbunga vingi vinatokea baharini lakini vikija nchi kavu havichukui muda mrefu vinapotea, pamoja na kuwa tunakitegemea kimbunga Jobo kufika huku kwetu, lakini hali inaweza kubadilika na kubadili mwelekeo kama ilivyokuwa kwa kimbunga Kenedy ambacho kiliishia pwani ya kusini mwa Afrika huko Msumbiji ingawa kilionekana kuja huku kwetu," alisema.




KHERI YA SIKU YA MUUNGANO! TANZANIA

Bodi ya wakurugenzi, Uongozi na wafanyakazi wote wa kampuni ya ujenzi wa reli ya SGR Tanzania - Yapi Merkezi, tunapenda kuwapogeza watanzania wote katika kusherehekea maadhimisho ya miaka 57 ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kheri ya siku ya muungano!

yapı merkezi

# RC asimulia alivyopambana kumfunga mbakaji

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amesimulia kesi ya ubakaji ambayo aliisimamia dhidi ya mwenye nyumba kumbaka mtoto wa mpangaji wake, mwanafunzi wa darasa la nne na kufanikisha kufungwa jela.

Akizungumza hivi karibuni kwenye kikao cha masuala ya ukatili wa kijinsia, mkoani humo, alisema tukio hilo lilitokea mwishoni mwa mwaka jana. Alisema mwanamume huyo mkazi wa Shinyanga, alikuwa na mahusiano ya kimapenzi na mama wa mtoto huyo, lakini akaiingiwa na tamaa na kumbaka mtoto wake.

Telack alisema baada ya kuona kesi hiyo inataka kuchezewa, aliingilia kati kuisimamia, na hatimaye mwanamume huyo alipatikana na hatia na hukumu yake ilitolewa Machi 3, mwaka huu na kufungwa jela miaka 30.

"Niliisimamia kesi hii mimi mwenyewe, kwa sababu nilishasema kwamba sitakubali mtoto wa kike apate unyanyasaji wa aina yoyoye ile ndani ya mkoa wangu, naipongeza Mahakama ya Wilaya ya Shinyanga kwa kumfunga jela mbakaji huyu miaka 30," alisema Telack.

"Hii ni aibu sana kwa huyu mwenye nyumba, yani ana mahusiano ya kimapenzi na mpangaji wake, lakini haridhiki ana mgeukia na mtoto wake ambaye ni mwanafunzi tena darasa la nne, niwambie tu wabakaji tutazidi kuwa wakali na mtafungwa jela," aliongeza.

Vile vile, alisema mkakati wa mkoa huo wa kuendelea kupambana kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya watoto, ni kuhakikisha kesi za aina hiyo zinafanyiwa kazi haraka, pamoja na kukamilishwa uchunguzi, ili wahusika wachukuliwe hatua kali za kisheria na liwe fundisho kwa wengine.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Msichana Intiatives, Rebeka Gyumi, wanaotetea haki za watoto, alipongeza Serikali ya Mkoa wa Shinyanga kwa jitihada wanazozifanya za kuhakikisha mtoto wa kike analindwa, pamoja na kupata haki zake ikiwamo elimu.

# RC abaini tatizo polisi doria usiku

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amesema baadhi ya askari polisi wanaofanya doria nyakati za usiku jijini Dodoma, wamekuwa wakitengeneza mazingira ya kupewa rushwa kwenye baa zinazozidisha muda uliopangwa na serikali.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Mahenge amewaonya huku akimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Josephat Maganga, kuzungumza na Mkuu wa Polisi wilayani humo ili kudhibiti vitendo hivyo.

Alitoa maagizo hayo baada ya kukutana na wafanyabiashara wa vileo ofisini kwake mwishoni mwa wiki na kuwasilisha kero wanazokumbana nazo kutoka kwa askari hao wanapozidisha muda wa kufunga maeneo yao ya biashara.

Akizungumza na wafanyabiashara hao, Dk. Mahenge alisema suala hilo amekuwa akilisikia mara nyingi kwamba kuna vikosi ukizindisha muda kidogo, wanafika na kutengeneza mazingira ya kupewa rushwa.

"Nikutake DC (Mkuu wa Wilaya) kakae na OCD, hili sasa limekuwa kero, na mimi nitaongea na RPC (Kamanda wa Polisi Mkoa), sitaki tena kusikia hili, OCD Wilaya ya Dodoma waonye askari wote wanaokuwa doria nyakati za usiku wenye tabia ya kuomba rushwa kwa wafanyabiashara na kuwataka waache mara moja kwani vitendo hivyo vinaliletea sifa mbaya Jeshi la Polisi," alisema.

Aliwataka wafanyabiashara hao kufuata matakwa ya leseni zao na kuepuka kutoa rushwa pindi wanapofanya makosa badala yake watoe taarifa na ama walipe faini au kuzungumza na mamlaka husika na siyo kutoa rushwa kwa askari polisi.

"Na ninyi sasa mfuate masharti ya leseni zenu kuepuka haya mambo, ukiambiwa funga baa saa tano au saa sita funga, umepewa leseni ya grocery, hakikisha unamfungia mteja anakwenda kunywea nyumbani, kama unataka uhudumie hapo tafuta leseni ya baa.

"Hapa tunapokea wageni mbalimbali kutoka nchi tofauti tofauti, tunataka wakija hapa wahudumiwe vizuri, kama ni hoteli na baa ahudumiwe vizuri ili hata akirudi kwao apakumbuke Dodoma, lakini siyo amekuja hapa usiku kapumzika anapigiwa kelele za muziki usiku mzima, hii siyo sawa kabisa, tunataka wawe salama," aliagiza.

Aliitaka halmashauri hiyo na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuandaa vipeperushi vyenye masharti yote na maonyo yanayohusu biashara ya vileo na kuvibandika kila eneo lenye biashara hiyo kusaidia kuwakumbusha wafanyabiashara.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema wameandaa mpango kabambe wa ardhi wa miaka 20 katika eneo lote la jiji ili kusaidia kuepusha migongano ya matumizi ya ardhi kwa kupanga kila eneo na matumizi yake kama makazi, biashara, viwanda na taasisi mbalimbali.

Alisema katika eneo la biashara ya vileo, wamiliki wake wamekuwa wakiuka masharti ya leseni zao kwa kuongeza biashara nje ya makubaliano au nje ya leseni, akitolea mfano kwamba anaomba leseni ya grocery lakini akikaguliwa anakutwa akiuza kama baa.

Meneja wa NEMC Kanda ya Kati, Frankline Rwezimula, alisema kuna sheria inayosimamia uchafuzi wa mazingira kwa njia ya sauti ambayo inafanya kazi katika viwanda, mitambo, magari na maeneo ya starehe.

Alisema mara kwa mara wamekuwa wakipokea malalamiko kutoka kwa wananchi wanaoishi maeneo jirani na sehemu za starehe kuwa wamekuwa wakipiga muziki kwa sauti ya juu jambo ambalo ni kinyume cha sheria.







**SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)**

**TAARIFA KWA WAAGIZAJI MAGARI KUTOKA NJE KUHUSU UWEPO WA MATAPELI**

**Dar es Salaam, 25 Aprili, 2021**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lina utaarifu umma kuwa limepokea malalamiko ya uwepo wa baadhi ya mawakala wasio waaminifu wanao wadanganya wateja wenye magari yaliyowasili bandarini kulipa gharama za ziada ili kuweza kutoa magari hayo.

Hivyo basi, TBS inapenda kuwataarifu na kuwatahadharisha waagizaji na wanaotoa magari bandarini kuwa;

1. Hakuna gharama zozote za ziada za utoaji magari baada ya ukaguzi bandarini tofauti na ada ya ukaguzi (Inspection fee).
2. Malipo yote ya ukaguzi ni lazima yalipwe kupitia mfumo wa kielektroniki (control number) na risiti lazima itolewe.

**Kwa maelezo zaidi tafadhali piga namba ya bure: 0800110827.**

**Imetolewa na:**

**Gladness H. Kaseka**
**MKUU WA KITENGO CHA UHUSIANO NA MASOKO**

TANGAZO

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA MAKAMU WA RAIS

# TAARIFA MAALUM YA MIAKA 57 YA MUUNGANO WATANGANYIKA NA ZANZIBAR

**1.0 UTANGULIZI**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania leo imetimiza miaka 57 tangu kuasisiwa kwake tarehe 26 Aprili, 1964. Muungano huu ambao uliunganisha zilizokuwa Dola mbili huru za Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, umetupatia mafanikio lukuki katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa ambayo yanaendelea kuwanufaisha wananchi wa pande mbili za Muungano kwa kuwapa fursa za kuishi kwa amani na kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muungano huu adimu na adhimu umeendelea kudumu na kimsingi umekuwa ndio nyenzo muhimu ya Utambulisho, Amani, Umoja na Mshikamano wa Taifa letu.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Sura ya 11 Ibara ya 47 (i), jukumu la kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kufuatilia utekelezaji wa siku hadi siku wa mambo yanayohusu Muungano yamekabidhiwa kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais ndiyo yenye dhamana ya kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa masuala yote ya Muungano na kuimarisha ushirikiano kwa mambo yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

Utekelezaji wa majukumu haya ya Kikatiba na Kisheria yamekasimiwa kwa Idara ya Muungano chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ilianzishwa rasmi mwaka 1998 kwa lengo la kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**3.0 MAFANIKIO**

Muungano huu umedumu kutokana na dhamira za dhati za umoja waliokuwa nao Waasisi wetu, sera makini za Serikali zote mbili za TANU na ASP na sasa CCM. Aidha, tumeshuhudia jitihada nyingi za viongozi wa awamu zote za kuhakikisha Muungano wetu unaendelea kudumu na kuimarika na kuwa Muungano wa mfano na wa kuigwa Barani Afrika na Duniani. Pia, Serikali zetu mbili zimeweka utaratibu wa kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazojitotokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano kupitia Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano ambayo imeendeleza utamaduni wa kukaa pamoja kutafuta ufumbuzi wa changamoto za Muungano.

Katika kipindi cha miaka 57 ya Muungano, tumeshuhudia mafanikio makubwa ya kujivunia kwa kuwa na Muungano wa kipekee uliodumu kwa muda mrefu Barani Afrika. Watanzania wamejenga umoja na misingi endelevu ya udugu baina yao, ikiwa ni uthibitisho kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar unaendelea kuimarika, pamoja na kuhakikisha kuwa uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar vinaenziwa. Vilevile, pande mbili za Muungano zimejenga mifumo ya kuendesha Serikali zake kwa uwazi chini ya misingi ya demokrasia na utawala bora. Misingi hiyo imeimarika kutokana na uelewa mzuri wa dhana ya uwajibikaji kwa viongozi wa ngazi zote.

Kwa kipindi cha miaka miaka mitano 2015 hadi 2019 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesimamia vizuri uchumi wetu, ambapo ulikua kwa wastani wa asilimia 7.0 kwa mwaka. Aidha, Pato ghafi la Taifa liliongezeka kutoka shilingi trilioni 94.349 mwaka 2015 hadi kufikia shilingi trilioni 139.9 mwaka 2019; Pia, Pato la Wastani la Kila Mtu liliongezeka kutoka shilingi 2,225,099 (sawa na dola za Marekani 1,022) mwaka 2016 hadi shilingi 2,577,967 (sawa na dola za Marekani 1,126.4) mwaka 2019. Mfumuko wa bei ulidhibitiwa kutoka wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2019 na kuongezeka kwa akiba ya fedha ya kigeni kutoka Dola za Marekani bilioni 4.09 mwezi Desemba 2015 (kiasi kinachotosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi 5.1) hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 4.8 mwezi Desemba, 2020 (kiasi kinachotosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi 5.6).

Vilevile, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 8.9 mwaka 2015 hadi Dola za Marekani bilioni 9.7 mwaka 2019; na pia kuvutia uwekezaji kutoka nje wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 16.2, sawa na zaidi ya shilingi trilioni 37 mwaka 2019 ukilinganisha na Dola za Marekani bilioni 13.7 mwaka 2015. Aidha, kwa Umasikini wa kipato ulipungua hadi kufikia asilimia 26.4 kwa takwimu za mwaka 2017/2018. Kwa upande wa mfumko wa bei, tunaendelea kuwa na mfumko wa bei ulio katika tarakimu moja.

Kwa upande wa Zanzibar, mafanikio yamepatika katika kusimaimia uchumi, ambapo katika kipindi cha mwaka 2011 – 2019, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.4. Kwa mwaka 2019, uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 7.0 na Mfumuko wa Bei umeendelea kubakia katika tarakimu moja. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Aprili, 2020 ulifikia asilimia 3.6.

Pia, tumeshuhudia kuimarika kwa miundombinu ya barabara, usafiri wa anga, usafiri wa majini na huduma za kijamii katika pande zote za Muungano. Vilevile, tumeendelea kutumia maliasili zetu vizuri zaidi kwa manufaa ya wananchi kuliko ilivyokuwa kabla ya Muungano. Mafanikio hayo yametokana na usikivu, utulivu, uzalendo, moyo wa kujituma na kujitolea na ushirikiano wa dhati wa viongozi na wananchi. Mafanikio haya, bila shaka, ndiyo yaliwezesha Tanzania kutangazwa kuingia kundi la nchi za uchumi wa kati kutoka kundi la nchi masikini mwezi Julai, 2020.

Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana, kumekuwa na baadhi ya changamoto ambazo kwa ujasiri mkubwa viongozi wa pande zote mbili za Muungano wanaendelea kuzipatia ufumbuzi. Juhudi hizi zilianza mara tu baada ya Muungano wetu mwaka 1964 ikiwa ni pamoja na kuundwa kwa Tume na Kamati kwa ajili ya kushughulikia changamoto za Muungano. Tume na Kamati hizo ni pamoja na:- Tume ya Dr. Salmin Amour 1984 ; Tume ya Jaji Nyalali 1990 ; Tume ya Mzee Edwin Mtei 1991 ; Kamati ya Shellukindo 1992 ; Tume ya Jaji Kisanga 1999 ; na Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano mwaka 2006.

**Mafanikio mbalimbali yamepatikana kutokana na utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati na Tume zilizoundwa na Serikali kama ifuatavyo: -**

i. Sheria kadhaa zimetungwa au kurekebishwa kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa mambo ya Muungano. Sheria ni pamoja na:-
   - Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sheria Na.13 ya 1995;
   - Sheria ya Uhamiaji, Na. 6 ya mwaka 1995 imetungwa na sasa watanzania wanaweza kwenda sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila vikwazo;
   - Sheria ya Mamlaka ya Kodi, Na. 11 ya 1995.
   - Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Na. 1 ya 1995.
   - Sheria ya Tume ya Pamoja na Fedha Na. 14 1996.
   - Sheria ya Biashara ya Bima ya Tanzania Na.18 ya 1996.
   - Sheria ya Usalama wa Taifa Na. 15 ya 1996;
   - Sheria ya Uraia Na.6 ya mwaka 1995;
   - Sheria ya Usalama wa Taifa Na. 15 ya mwaka 1995; na
   - Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu, Sheria Na. 5 ya mwaka 2020.

ii. Tawi la Benki Kuu ya Tanzania limejengwa Zanzibar ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefungua akaunti yake Benki Kuu na inaendelea kupata huduma za kibenki ikiwepo mikopo na ushauri juu ya kukuza uchumi kwa wananchi wa Zanzibar.

iii. Muungano wetu umeiwezesha nchi kuwa shwari, salama na tulivu. Tumeweza kulinda uhuru wetu na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar dhidi ya matishio mbalimbali. Umoja wetu na mshikamano ndani ya Muungano pamoja na uwezo na weledi tulioujenga kwa vyombo vya ulinzi na usalama vya Serikali ya Muungano ndiyo siri ya mafanikio yetu;

iv. Mfumo wa vyama vya siasa umepewa nguvu na Sheria ya Vyama vya Siasa (The Political Parties Act) Sura Namba 258, inayovitaka vyama hivyo kuwa na sura ya kitaifa. Mfumo wa vyama vingi vya siasa, umeimarisha demokrasia, uhuru wa kutoa maoni na uwazi katika uendeshaji wa shughuli za umma ikiwa ni pamoja na masuala ya Muungano. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini ilianzishwa mwaka 1992 ambayo ina Ofisi kuu Dodoma na Ofisi ndogo Zanzibar. Hadi sasa, vyama vya siasa 19 vimepata usajili wa kudumu.

v. Kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano: Serikali zote mbili zimeweka utaratibu wa vikao vya kisekta vya ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano. Lengo la kufanya vikao hivyo ni kuimarisha ushirikiano kwa manufaa ya Watanzania. Vikao hivyo vimekuwa vikijadili masuala ya kisekta, kubadilishana ujuzi, utaalamu na uzoefu kupitia mafunzo, masuala ya sera na ushiriki katika masuala ya kimataifa. Ushirikiano huu ni muhimu kwa kuwa unasaidia kuzitafutia ufumbuzi kwa haraka na kwa ufanisi changamoto za Muungano na za kisekta zilizopo na zinazojitokeza. Tathmini inaonesha Wizara za Kisekta zinapokutana changamoto zinapungua na Muungano unazidi kuimarika.

   Jumla ya vikao 194 vya ushirikiano vimefanyika katika kipindi cha 2000 - 2021. Sekta zilizokutana ni Mawasiliano na Uchukuzi, Serikali za Mitaa, Miundombinu, Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Nishati, Maliasili na Utalii, Viwanda, Biashara, Masoko, Utumishi, Uratibu wa Shughuli za Serikali, Katiba na Sheria, Utawala Bora, Afya, Elimu, Habari na Utamaduni, Uchumi na Fedha.

vi. Kuelimisha umma kuhusu Muungano: Ili kuwa na jamii yenye uelewa wa masuala ya Muungano na kuweza kuuenzi na kuutetea, Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa ikichukua jitihada mbalimbali kuelimisha umma kuhusu Muungano. Wananchi wamekuwa wakielimishwa kupitia vipindi vya Redio na Televisheni, Makala Magazetini, Semina, Warsha, Makongamano, Maonesho ya Kitaifa, Ziara za viongozi, machapisho mbalimbali na mitandao ya kijamii.

vii. Miradi ya Maendeleo: Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kushirikiana katika kuibua na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Miradi hii imewawezesha wananchi wa pande zote mbili za Muungano kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kuongeza ajira za muda kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Utekelezaji wa miradi hiyo umefanikiwa kuinua hali ya wananchi, kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato na kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii wa pande zote mbili za Muungano.

**Miongoni mwa miradi na programu zilizowahi kutekelezwa pande mbili za Muungano na kukamilika ni pamoja na: -**

- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania Social Action Fund – TASAF) TASAF I, TASAF II na TASAF III Awamu ya Kwanza;
- Programu ya Usimamizi wa Bahari na Pwani (Marine and Coastal Environmental Management Programme - MACEMP);
- Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Sekta ya Mifugo (Agricultural Sector Development Program – ASDP);
- Agricultural Sector Development – Livestock – ASDP – L, Agricultural Sector Support Program – ASSP;
- Programu ya Changamoto za Milenia (Millenium Challenge Account Tanzania – MCA – T);
- Mradi Shirikishi wa Programu za Maendeleo ya Kilimo (Participatory Agricultural Development Program – PADEP);
- Mradi wa Udhibiti wa Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Programme – SWIOFISH); na
- Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Fedha Vijijini (Market Infrastracture, Value Addition and Rural Finance - MIVARF)

**Miradi na programu zinazoendelea kutekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar ni pamoja na:-**

- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania Social Action Fund – TASAF III) Awamu ya Pili;
- Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga (Expanded Rice Production Project – ERPP);
- Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Maeneo ya Pwani - LDCF;
- Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini nchini Tanzania (Ecosystem Based Adaptation for Rural Resilience in Tanzania - EBARR)
- Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA);
- Mpango wa kupanua usikivu shirika la utangazaji Tanzania (TBC);
- Mradi wa uboreshaji wa Elimu kupitia Global Partnership for Education; na
- Mradi wa sumu kuvu.

viii. Ujenzi wa Taasisi za Muungano Zanzibar: Serikali imekamilisha ujenzi wa wa Tawi la Benki Kuu lililopo Gulioni, Zanzibar; Ofisi ya Makamu wa Rais, Uhamiaji, Makao Makuu na Ofisi za Bunge Tunguu, Zanzibar; Mamlaka ya Utabiri wa Hali ya Hewa, eneo la Uwanja wa Ndege, Zanzibar; Makao Makuu ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu, Fumba; na Taasisi ya Sayansi za Bahari iliyoko Buyu. Aidha, Tume ya Mabadiliko ya Katiba imefungua Ofisi Kikwajuni, TANTRADE na NIDA zimefungua Ofisi Zanzibar, Sekretarieti ya Ajira imefungua Ofisi eneo la Shangani, TAEC na COSTECH zina Ofisi za kudumu Maruhubu, Zanzibar. Pia, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; Baraza la Taifa la Mitihani la Taifa; Idara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; Mamlaka ya Usafiri wa Anga; Kampuni ya Posta Tanzania; Kampuni ya Simu Tanzania; Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa; Tume ya Uchaguzi ya Taifa; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Mamlaka ya Mapato Tanzania; Tume ya Pamoja ya Fedha; Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano; na Mamlaka ya Bima Tanzania

**Lengo la kujenga na kufungua Ofisi na Taaisisi hizo ni kusogeza karibu huduma kwa wananchi wa Zanzibar.**

**4.0 CHANGAMOTO**

Muungano umepitia vipindi vyenye matukio mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yaliyotokea ndani na nje ya nchi na ambayo kwa njia moja au nyingine, yaliathiri uendeshaji wa shughuli za Muungano. Miongoni mwa hayo ni: -

i. Kuvunjika kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1967;
ii. Kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977;
iii. Vita dhidi ya Iddi Amini wa Uganda mwaka 1979;
iv. Kuyumba kwa uchumi wa Dunia miaka ya 80;
v. Kulegezwa kwa masharti ya biashara na kuanzishwa sera ya uchumi huria; na
vi. Kuanzishwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa mwaka 1992.

Changamoto nyingine ni pamoja na uwepo wa tofauti ya Sheria kwa pande mbili za Muungano, hukwamisha utekelezaji wa baadhi ya maamuzi yanayofikiwa katika kutatua changamoto za Muungano. Hata hivyo, inapotokea changamoto ya tofauti ya sheria, Serikali zetu mbili zinashirikiana katika kuzioanisha Sheria zinazokwamisha utekelezaji.

Hatua zilizochukuliwa

Mifumo imara iliyowekwa ya kujadili na kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoukabili Muungano wetu, imewezesha pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano kupiga hatua kubwa kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na hivyo kupata sifa kubwa kimataifa.

Kuundwa kwa Tume na Kamati zilizopewa majukumu ya kuchunguza na kubainisha changamoto za Muungano na kutoa mapendekezo Serikalini, ni miongoni mwa juhudi kubwa zinazochukuliwa katika kutatua changamoto zinazojitokeza. Tume na Kamati hizo ni pamoja na Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano iliyoundwa mwaka 2005 na kuanza vikao mwaka 2006, imekuwa ni nyenzo muhimu katika kuimarisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioasisiwa mwaka 1964. Vikao vinavyojumuisha wajumbe kutoka pande zote mbili za Muungano vimekuwa vikifanyika katika ngazi za Wataalamu, Makatibu Wakuu, Mawaziri na Kamati ya Pamoja ya SMT na SMT chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuhakikisha changamoto zote zinatafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utatuzi wa changamoto zilizojadiliwa na kupatiwa ufumbuzi tangu mwaka 2006, Serikali zetu mbili zimeandaa Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano ili kuongeza kasi ya uratibu wa vikao na ufuatiliaji wa maagizo, maelekezo na maamuzi yanayotolewa katika vikao hivyo.

Utaratibu huu, ulipitishwa kwenye Kikao cha Kamati ya Pamoja cha tarehe 9 Februari, 2019, unaimarisha na kurasimisha utaratibu wa vikao vya pamoja na kuweka muda kwa vikao vya kila ngazi. Utaratibu huo pia umeainisha Kamati mbili ambazo ni Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala zilizopewa jukumu la kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazohitaji utatuzi wa haraka badala ya kusubiri utaratibu wa kawaida wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ. Kamati hizi huwasilisha taarifa zake kwenye vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ.

Tangu mwaka 2006, vimefanyika vikao kumi (11) vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ. Vikao hivi hutanguliwa na vikao vya Mawaziri, Makatibu Wakuu na wataalamu wa kisekta kutoka Serikali zote mbili. Katika vikao hivyo changamoto mbalimbali hujadiliwa na kupatiwa ufumbuzi.

**Hoja zilizopatiwa ufumbuzi ni:-**

i. Utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;
ii. Utekelezaji wa Merchant Shipping Act katika Jamhuri ya Muungano na Uwezo wa Zanzibar Kujiunga na International Maritime Organisation (IMO);
iii. Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;
iv. Uwezo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Kukopa Ndani na Nje ya Nchi;
v. Misamaha ya Mikopo ya Fedha kutoka IMF;
vi. Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asili;
vii. Ushiriki wa SMZ katika masuala mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda;
viii. Kuondoa kodi katika unga wa maziwa toka Zanzibar kuja Tanzania Bara;
ix. Gharama za Kushusha Mizigo (Landing Fees);
x. Tatizo la Usimamizi wa Ukokotoaji na Ukusanyaji wa Kodi kwenye Huduma za Simu unaofanywa na ZRB;
xi. Kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete – Pemba (Serikali imesaini Mkataba na Saudi Fund tarehe 19 Aprili, 2020);
xii. Kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi;
xiii. Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu;
xiv. Kuzuiwa kwa bidhaa ya sukari inayozalishwa katika Kiwanda cha Mahonda Zanzibar kuingia katika soko la Tanzania Bara; na
xv. Upatikanaji wa fursa za ushiriki wa Zanzibar katika miradi ya maendeleo ya viwango na ubora wa bidhaa na maendeleo ya wajasiriamali.

**Hoja zilizo katika hatua mbalimbali za kupatiwa ufumbuzi ni:-**

i. Hoja za fedha; na
ii. Biashara baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Serikali zote mbili SMT na SMZ zinaendelea kushughulikia changamoto za Muungano kadri zinavyojitokeza.

**5.0 MAADHIMISHO**

Tunapoadhimisha miaka 57 ya Muungano wetu tunaongozwa na Kauli Mbiu isemayo: ''Muungano Wetu ni Msingi Imara wa Mapinduzi ya Kiuchumi, Tudumishe Mshikamano Wetu''. Hivyo ni vema, sote tuendelee kuulinda, kuuenzi na kuudumisha Muungano wetu adimu na adhimu kwa manufaaa yetu sote.

**6.0 HITIMISHO**

Mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi cha miaka 57 ya Muungano wetu yametokana na jamii yenye umoja, mshikamano na isiyo na ubaguzi wa aina yoyote. Watu wa pande zote mbili za Muungano wanaishi na wanafanya kazi zao za kujiletea maendeleo katika sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kubughudhiwa.

Pia, mafaniko hayo yanatokana na ushirikiano mzuri kati ya viongozi na wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Kwa muktadha huo, mafanikio hayo siyo ya kubezwa hata kidogo na yanapaswa kulindwa, kudumishwa na kuendelezwa kwa nguvu zote.

**Selemani Saidi Jafo (Mb.)**
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO NA MAZINGIRA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vurugu, fujo za mashabiki hazina tija katika michezo

**MASHABIKI** ni watu muhimu sana katika viwanja vya michezo mbalimbali kokote hapa duniani.

Hili tumelishuhudia na kudhihirisha umuhimu wao katika kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa COVID 19, ambapo serikali na nchi mbalimbali zilisitisha mashabiki kuhudhuria viwanjani.

Katazo hilo mbali na kuzikosesha timu na wanamichezo mapato ya kujiendesha, lakini lilipunguza shangwe kwa mashindano mbalimbali yaliyokuwa yakiendelea mpaka mabingwa walipopatikana na hatimaye kujifunza kitu kipya.

Ilionekana wazi kukosekana mashabiki hao viwanjani kulipunguza ushindani kwa baadhi ya mechi kwa sababu wachezaji wake walikosa watu wa kuwahamasisha na kucheza katika viwango vya juu kama walivyozoeleka.

Lakini mashabiki hao ambao ni sawa na mchezaji wa 12 katika timu kama wanavyoitwa kwenye upande wa mchezo wa soka, bado wanatakiwa kufahamu mipaka na hazi walizonazo wanapokuwa kwenye viwanja kwa ajili ya kuzishabikia au kuziunga mkono klabu wanazozipenda.

Katika siku za hivi karibuni tumeshuhudia mashabiki wakivuka mipaka kwa kuingilia majukumu ya makocha au ya viongozi wanaoongoza klabu au vyama vya mikoa kwa sababu tu mambo hayaendi kama walivyotarajia.

Tunapenda kuwakumbusha pamoja na umuhimu wao, lakini ni vyema mashabiki wakafahamu mipaka yao na kujiepusha kuziingiza timu au wanamichezo wanaowashangilia kwenye wakati mgumu wa kufungiwa au kutozwa faini.

Katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Gwambina FC dhidi ya mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba kutoka jijini Dar es Salaam kulionekana vitendo vya mashabiki kumrushia shupa mwamuzi msaidizi namba moja kwa ishara ya kutokubaliana na uamuzi alioufanya wa kukataa bao lililofungwa na mchezaji wao, Joash Onyango.

Kwa kufanya hivyo, mashabiki hao wanaiweka timu yao kwenye hatari ya kutozwa faini au adhabu nyingine kubwa, hali ya kuwa walipaswa kutulia na kuacha viongozi wao kuchukua njia sahihi ya kuwasilisha malalamiko yao katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa sababu kitendo cha kumpiga mwamuzi au waamuzi hakiwezi kubadilisha matokeo.

Katika dunia hii ya utandawazi ambapo mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara zinaonyeshwa mubashara, idadi kubwa ya matukio yanayofanyika uwanjani huonekana kupitia kamera zilizoko kwenye viwanja hivyo, na kwa sababu hiyo huu ni wakati wa mashabiki kujirekebisha au kuacha kabisa kujichukulia hatua mkononi.

Vurugu au fujo hizo za viwanjani unaweza ukaziangalia katika ngazi ya Ligi Kuu, lakini kumbe wasimamizi wa mchezo huo wakubwa katika ngazi ya CAF au FIFA wanaweza kuchukua picha hizo za vurugu na hatimaye kuinyima Tanzania haki ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya kimataifa pale itakapoomba kwa ushahidi kwamba nchi hii si salama.

Nipashe inawasisitiza mashabiki, viongozi na wachezaji kuimarisha nidhamu wanapokuwa uwanjani kwa ajili ya kuiongezea heshima na thamani Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo msimu huu imetoa timu moja iliyoingia katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa mashabiki wa Simba, wao ndio wanatakiwa kuongeza utulivu kwa sababu wapinzani wa timu yao (timu nyingine saba zilizotinga robo fainali), kwa sasa wanawafuatilia wawakilishi hao kwenye kila mchezo wanaocheza ili kuwapeleleza kwa ajili ya kukabiliana nao kwenye hatua hiyo inayofuata.

Tunawakumbusha katazo la kutocheza na mashabiki lilivyopunguza shamrashamra katika baadhi ya michezo kwenye msimu uliopita na huu, hivyo tukumbuke utulivu wa mashabiki huisaidia timu wanayoishangilia kuvuna matokeo chanya na si kujiweka kwenye mazingira ya kuadhibiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera sana Mbeya Kwanza, lakini...

Na Adam Fungamwango

**WAKATI** timu mbili za Mbeya, Ihefu SC na Mbeya City zikitapatapa mkiani kutaka kujinusuru kuepuka kushuka daraja, timu nyingine ya jijini humo, Mbeya Kwanza tayari imefakikiwa kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara.

Timu hiyo itaanza kuonekana rasmi kwenye Ligi Kuu Bara katika msimu ujao wa 2021/22. Haijalishi kama Ihefu na Mbeya City zitashuka zote au moja wapo. Ikiwa zote zitafanikiwa kubaki basi mkoa wa Mbeya itakuwa na timu tatu, tukiacha Prisons ambayo yenyewe iliamua kwenda kuweka kambi yake mjini Sumbawanga mkoani Rukwa.

Iliichapa African Sports ya Tanga bao 1-0 kwenye Uwanja wa Mabatini mkoani Pwani, lililofungwa na Willy Edger dakila ya 75, na ushindi huo ukawafanya kufikisha pointi 38 kwenye Kundi A na kuwaacha African Sports kwenye nafasi ya pili wakiwa na pointi 28.

Mbeya Kwanza ni timu iliyoanzishwa mwaka 2012 ikiitwa Coca Cola Kwanza, lakini mwaka 2014 ilibadilishwa na kuitwa Mbeya Warriors wakati huo ikishiriki Ligi ya Mabingwa wa Mkoa.

Tunaipongeza timu ya Mbaya Kwanza kwa kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara na nadhani wiki hii kutakuwa na sherehe kubwa jijini Mbeya kwa timu hiyo kufanikiwa kupanda.

Viongozi mbalimbali na wananchi watamiminika na kutoa sifa kwa viongozi na wachezaji, huku kila mmoja akijipa sifa ya kuwa mmoja wa waliofanikisha timu kupanda. Lakini pamoja na hayo kuna angalizo

Hata hivyo, kupanda Ligi Kuu kuu ni jambo moja na kushiriki ni jambo lingine.

Kumekuwa na timu nyingi zinapanda Ligi Kuu Bara kwa nderemo, chereko na hoi hoi, lakini zinapokuwa kwenye ligi hiyo zinakuwa kama ni timu zilizotelekezwa.

> **Iliichapa African Sports ya Tanga bao 1-0 kwenye Uwanja wa Mabatini mkoani Pwani, lililofungwa na Willy Edger dakila ya 75, na ushindi huo ukawafanya kufikisha pointi 38 kwenye Kundi A na kuwaacha African Sports kwenye nafasi ya pili wakiwa na pointi 28.**

Kushiriki Ligi Kuu Bara kuna gharama kubwa mno, hivyo sasa viongozi wa Mbeya Kwanza wakati wanasherehekea, wapate muda wa kuanza kujiuliza na kuweka mipango watacheza vipi ligi hiyo ya juu nchini katika msimu ujao.

Isije ikawa timu imepanda, lakini baadaye ikawa ni mlalamiko tu kila kukicha ya mishahara na posho za wachezaji, na mambo mengine mengi wanayofanana na hayo.

Mambo ya kutegemea wananchi wa mkoa husika kuchangishana yameshapitwa na wakati.

Ni wakati pia wa kuanza kusaka wachezaji wazoefu wa wenye viwango vya hali ya juu kwenye Ligi Kuu, ili yasije yakawakuta kama ya Ihefu FC ambayo ilidhani kucheza na wachezaji iliotoka nao Ligi Daraja la Kwanza ingewasaidia.

Ni uzalendo ambao umewaponza na kuwafanya hivi sasa kupigana kwa hali yoyote ile ili isishuke daraja.

Wakati nikitoa salamu za pongezi kwa Mbeya Kwanza, na kuipa tahadhari isije kichwa kichwa kwenye Ligi Kuu, naligeukia Shirikisho la Soka nchini (TFF) kuiangalia sana ligi hiyo ambayo tayari kuna malalamiko yameshaanza juu ya visa vya upangaji matokeo na uendeleo.

Tumesikia timu za Mbao, Geita Gold na Pamba ya Mwanza zikilaumiana kufanyiana hujuma kila moja ikiilaumu nyingine.

Ni wakati wa TFF kuitupia macho ligi hii kwani kwa miaka mingi imekuwa ikilalamikiwa lwa baadhi ya timu kufanya mipango ili kupanda Ligi Kuu.

Tayari Mbeya Kwanza imepanda, tunategemea sasa timu za Kundi B, pamoja na zile zitakazoshika nafasi za pili. Hivyo umakini wa waamuzi pamoja na TFF kufuatilia kwa makini mechi hizi unahitajika ili kusiwepo na upangaji wa matokeo.

MUUNGANO 1964 HADI 2021

# Una sura pana kuvuka ya vitabuni

## ●Urafiki wa Nyerere- Karume, sasa wa wote
## ●Mtaji Kiswahili ndiyo 'grisi' iliyofanikisha

**Na Peter Orwa**

LEO hii ni shamrashamra ya sherehe ya Muungano wa Tanganyika na Unguja, ikitimia miaka 57. Ni faraja iliyobeba mustakabali mpana na umri mrefu, waliozaliwa wakati wa tukio hilo, leo ni wazee umri wao uko katika 'tia maji tia maji' kuelekea kustaafu.

Muungano huo una mzizi mrefu, kisheria na yasiyo kiseria, kwani hata kabla ya kuungana, ni jamii zilizohusiana kihistoria kurejea hata nyuma katika nyendo za utumwa katika ukanda huo jirani, biashara hiyo chafu ikiwa na uhusiano katika bandari za Bagamoyo na Unguja.

Ishara nyingine ya wazi ni ukaribu, hasa inaposhuhudiwa safari ya ndege kati ya Unguja na Dar es Salaam, ni mwendo wa robo saa pekee, huku Tanga na Pemba ni usawa wa 'ng'ambo ile ya bahari!'

Hapo ndipo katika harakati viongozi wa kisiasa, Mwalimu Nyerere wa TANU na kaka yake Abeid Amani Karume, walihusiana kwa karibu, wakiwa marafiki hasa, kabla na baada ya uhuru wao kati ya mwaka 1961 hadi 1964.

Ndani ya hapo kunaangaliwa Muungano wa kinasaba, lugha kuu ya pande hizo mbili zikiwa Kiswahili, ambayo hata katika mustakabali wa kimataifa, ndiko kwenye mzizi mkuu wa umahiri duniani, kabla na baada ya uhuru kwa matumizi ya kawaida, sheria na taaluma.

Kwa maana hiyo, hata Muungano wa urafiki wa Mwalimu Nyerere na Karume, unaangukia mtazamo kwamba waswahili maswahiba, waliokuwa katika sura pana kuwakilisha nafsi za watokako Bara, pia Visiwani.

YALIYOJIRI 1964

Hivyo basi, uwasilishaji wa kilichojiri tarehe na siku kama ya leo, katika mwaka 1964 ilikuwa ni kutimiza kisheria na katika sura maalum, kilichokuwapo mapema, kijamii baina ya wakazi wa Tanganyika na Zanzibar.

Hata ikirejewa hotuba za Hayati Mwalimu Nyerere, alikuwa anamkumbuka mbia wake Karume, akimtunuku sifa ya 'uamuzi wa kijeshi' kwani wakati Nyerere akimtaka waandae namna watakavyojipanga kuongoza nchi, Karume alimpa jibu la papo kwa hapo: "Wewe (Nyerere) Rais, mimi (Karume) Makamu, tuanze kazi."

Ni muda mfupi baada ya hapo ndani ya kipindi hicho, upande wa Tanzania Bara ulikuwa unatekeleza Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 1964 hadi 1965.

Moja ya mikakati ilikuwa kuasisiwa ujenzi nyumba bora kwa mikopo ya gharama nafuu mwaka 1966, ambayo ilishuhudiwa katika miji mingi jijini Dar es Salaam, ikitawaliwa makazi kama ya Temeke, Ilala, Magomeni na Mwananyamala.

Hiyo pia ilifanyika kwenye makazi ya maghorofa Michenzani, vivyo hivyo kisiwani Pemba, hali iliyoonyesha miradi ya kufanana majengo hayo na yanayomilikiwa na Shirika la Nyumba Tanzania (NHC) kama Tandika na Ilala, Dar es Salaam, mjini Morogoro na Mbeya.

Ni picha inayoweka wazi namna kunavyowiana ushirikiano au Muungano wa mawazo, katika miradi ya maendeleo kitaifa.


Ni mustakabali wa ushirikiano katika Muungano uliopiga hatua katika ushirika wa mengi ambayo hayakupatikana upande mmoja, yalihudumia upande mwingine.

Itakumbukwa katika huduma ya tiba, Zanzibar ilikuwa haijafikia hatua ya kuwa na hospitali kubwa kama Muhimbili, ambayo tayari ilishakuwa na sifa ya kuwapo hata kabla ya uhuru wa Tanganyika.

Sehemu kubwa ya Wazanzibari tangu wakati huo wanaendelea kunufaika nayo hadi sasa, hali kama hiyo ikichukua picha pia katika ngazi ya elimu ya juu.

Hata hivyo, hadi sasa kuna utekelezaji wa mipango mkakati wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imeendana kuanzishwa Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) na uoanuzi wa Hospitali Kuu ya Mnazi

INAENDELEA UK. 8



Mwalimu Juiius Nyerere, alipokutana na Shekhe Abeid Karume.
**PICHA: MTANDAO.**




# Una sura pana kuvuka ya vitabuni

INATOKA UK. 7

Mmoja, mjini Unguja inayofanyiwa upanuzi mkubwa kukidhi mahitaji ya wakazi wake.

Itakumbukwa, aliyekuwa msomi na mwanasiasa maarufu wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, Maalim Shariff Hamad, njia zao mpango elimu ya Muugano na kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kisha akaivishwa kisiasa ndani ya Zanzibar.

Mengi yaliyo na sura ya urafiki wa kisiasa na kiuchumi yanabeba hali ya kufanana kwa kina, huku uswahiba wa Nyerere na Sheikh Karume, hata baada ya kifo chake mwaka 1972, uliendelezwa na mrithi, Aboud Jumbe Mwinyi na wengineo katika mnyororo mrefu wa historia ya uongozi Visiwani.

**SURA YA SIASA**

Hatimaye ilipotimu mwaka 1977, pande mbili ziliingia ubia wa kisiasa kuimarisha sura ya Muungano Afro Shiraz na TANU, ilipoungana na kuunda Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Ni hatua mojawapo inayounda tafsiri pana ya Muungano wa sasa, ikiteka mustakabali wote wa siasa kuwa katika lugha na itikadi zinazofana.

Hapo kulishuhudiwa mapana ya uswahiba wa Nyerere na Karume, kwa namna viongozi wa chama walivyoingiliana, sura za utendaji na uteuzi ndani wa kisiasa.

Kuna wakati, hata Rais Mstaafu Jakaya Kikwete, katika historia yake aliweka wazi kwamba moja ya maeneo yaliyomuivisha katika uzoefu wa kazi yake, akiwa mwanajeshi na kamisaa wa kisiasa katika chama (kwa mujibu wa sheria wakati huo), ni kituo cha kazi Zanzibar.

Ndiyo tasfri inayodumu hata katika mfumo wa uongozi ndani ya CCM na badahi ya vyama vingine vya kisiasa, mathalan makamu wenyeviti wanakuwa wawili, mmoja wa Zanzibar, mwingine Bara.

Hiyo inajitokeza hata katika historia ya uongozi wa nchi tangu kung'atuka Mwalimu Nyerere,



Mwalimu Juiius Nyerere, aliposaliamiana na Shekhe Abeid Karume, katika Uwanja wa ndege. Picha ya chini, walipokuwa pamoja katika moja ya matukio. **PICHA: MTANDAO.**



CCM katika orodha viongozi watano wa Muungano waliomfutia hadi sasa, wamo wawili watokao Zanzibar, akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan.

Pia, kuna kikuu katika utamaduni huo wa uongozi kupishana kama ilivyo katika ngazi ya juu ndani ya CCM, Rais atokaye upande mmoja wa Muungano, makamu anatoka upande mwingine wa Muungano.

Darasa la wazi ni kwa Rais Samia aliyekuwa Makamu katika awamu ya tano, katika nafasi ya sasa, makamu wake, Dk. Philip Mpango anatoka Bara.

Vivyo hivyo, kuna historia hata wakuu waliobahatika kuongoza taifa katika ngazi za juu, wana chimbuko la kuanzia ama Baraza la Mapinduzi na SMZ au Bunge la Muungano na serikali yake.

Mathalan, Rais Ali Hassan Mwinyi, alishatumikia Bunge la Muungano na uwaziri, kabla ya kuwa Rais wa SMZ na kisha kuiongoza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, huku mwanawe, Rais wa SMZ Dk. Hussein Ali Mwinyi, alishakuwa Mbunge Bara na akahamia jimbo lililoko Unguja, sasa ni Rais wa SMZ.

Pia, katika kada ya siasa, ACT - Wazalendo chama kipya katika ulingo wa siasa, muasisi wake Zitto Kabwe, ametumia vyema mtaji wa mwanasiasa mwandamizi Maalim Seif Shariff Hamad, kutikisa katika katika siasa za uchaguzi Zanzibar, baada ya kujiengua kutoka CUF, chama alichokiasisi.

Ni mtaji uliopa ACT - Wazalendo na Zitto mwenyewe umaarufu mkubwa Zanzibar, akiwa na kundi kubwa la waliokuwa makada, pia wanasiasa waandamizi wa CUF, ikiwa na mwanachama wake, Makamu wa Rais wa SMZ, Othman Masoud Othman

Leo hii chama CUF kimekwezwa na kina heshima ya kipekee kitaifa, kwa mtaji mkubwa wa Muungano, ikiinuliwa na vigogo kutoka Zanzibar, ambao wengi sasa wamejiengua kuingia ACT -Wazalendo mwaka jana.

Hata Mwenyekiti wake wa sasa, Profesa Ibrahim Lipumba, ana mzizi wa kukwea kisiasa, kutokana na historia ya ukaribu wake na aliyekuwa Katibu Mkuu, Maalim Seif Shaiff Hamad, rafiki wa tangu masomoni.

**BIASHARA**

Katika uhalisia wa uchumji wa chini na ujasiriamali, Wazanzibari, ambao kimsibgi wana asili ya biashara, ana mchango mkubwa katika kubadili biashara na uzaslishaji ngazi ya chini.

Kwa kutimia fursa za Muungano, wengi kutola Unguja na Pemba wameingia mtaji na kuhodhi mianya ya biashara, ikiwa imehamasika kama sera za nchi zinavyohimiza

Mathalan, katika uzalishaji mpunga nchini, wakuu wanahodhi nyendo hizo kuanzia kuwekeza kwa mkataba maalum na wazalishaji shambani hadi ununuzi wake, wanatoka Zanzibar, uhalisia ukishuhudiwa maeneo kwenye mashamba ya Kyela la Mbarali.

Vivyo hivyo, upande viswani kunadumu kuwa wateja wakuu wa bidhaa nyingi kutoka bara ambazo hazizalishwi huko, huku upande wa pili, kuna bidhaa za kimataifa zinazotakiwa hadi bara kutoka nje ya nchi, mfano mafuta ya kula yanapitia Unguja kutoka Uturuki, zikiwa na anwani rasmi ya kampuni za Zanibar.

Katika utalii, ndiyo ubia mkubwa wa kibiashara unaonekana ikizingatiwa sekta hiyo ni moyo wa uchukuzai wa SMZ.

Hadi sasa ndege nyingi za kimataifa ratiba zake ni kati ya Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam na Abeid Aman Karume, kabla hazijaendelea.

HABARI KITAIFA

# WMA waaswa kuhusu rushwa

Na Mwandishi Wetu

WAFANYAKAZI wa Wakala wa Vipimo (WMA),wametakiwa kufanya kazi kwa weledi na ubunifu na kuacha vitendo vya rushwa ambavyo vimekuwa vikiharibu sifa,ukandamizaji wa wateja na kusababisha Serikali kupoteza mapato yake.

Aidha Menejimenti ya WMA imetakiwa kuendelea kufanya kazi kwa kasi ili kuwafikia walengwa kwa kukagua vipimo vingi na kuongeza kasi ya ukusanyaji wa maduhuri kutoka Sh. bilioni 27 za sasa na kufikia zaidi ya sh. bilioni 30.

Wito huo umetolewa jana mkoani Pwani na Mwenyekiti wa Bodi ya WMA, Mhandisi Dk. Adelhelm Meru kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara wa ya Viwanda na Biashara, Dotto James, wakati akifungua mkutano wa 29 wa Baraza la Wafanyakazi wa WMA wenye lengo la kujadili Mpango na Bajeti katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22.

Alisema kwa miaka mitano, WMA imeweza kuongeza vipimo vilivyokaguliwa kutoka 700,000 kwa mwaka 2015 hadi kufikia 900,000 kwa mwaka 2020 ikiwa ni ongezeko la asilimia 40.

Mhandisi Dk. Meru alisema kwa upande wa ukusanyaji maduhuri, WMA imeweza kuongeza ukusanyaji wake kutoka Sh.bilioni 19.5 kwa mwaka 2015 hadi Sh. bilioni 27 mwaka 2020 sawa na asilimia 40.

Aidha, alisema kupitia mkutano huo, Baraza hilo litapitia bajeti ya WMA kwa mwaka 2021/22, kwani kupitiwa kwa bajeti hiyo ni utamaduni uliozoeleka.

"Tunatambua kwamba ili uongozi uweze kuendana na wafanyakazi wenzao ni vizuri kuwashirikisha wafanyakazi katika masuala haya ya bajeti, hii ni hatua moja inaonesha wakala wa vipimo haiwaachi mbali wafanyakazi wake kushirikiana nao katika mambo yote yanayohusu hatima ya Wakala wanayoongoza,"alisisitiza Dk. Meru.

Alisema Baraza hilo litapitia bajeti na kuangalia mapendekezo ambayo yamefanywa na uongozi, bajeti hiyo itawekwa wazi ili kusudi wafanyakazi au wawakilishi wao wapate fursa ya kupitia ,kuchambua na kuweza kutoa maboresho au mapendekezo ambayo yataboresha zaidi bajeti hiyo. "Mara nyingi bajeti ni hatima ya wafanyakazi wote na ni muongozo utakaowaongoza watendaji kwa muda wa mwaka mzima, hivyo ni muhimu kutumia nafasi hii kuangalia kwa uwazi na umakini ili mwisho wa siku kiweze kutoka kitu ambacho ni kizuri hata kitakachoenda wizarani au Bungeni kiende kitu ambacho kimebeba mambo yote matakwa na mahitaji ya wafanyakazi wote,"alisema.

Aidha alisema amepata fursa ya kutembelea sehemu mbalimbali katika Wakala hiyo na kujionea namna WMA inavyofanya kazi na kuangalia ripoti zao kuwa imeimarika na inafanya vizuri katika kazi.

Kwa Upande wake Kaimu Ofisa Mtendaji wa WMA, Stella Kahwa, alisema lengo kuu la kikao hicho cha baraza ni kujadili bajeti ya WMA ambapo Wakala ya vipimo ina mikoa 29.

Alisema bajeti hiyo inayofanyiwa maboresho kuanzia ngazi ya mkoa. "Bajeti lazima iwe shirikishi na ikiwa shirikishi ni rahisi kutekelezeka,hiki tunachojadili ni majumuisho ya bajeti ndogo ndogo zilizotengenezwa kuanzia ngazi ya mkoa,"alisema

Alisema katika kikao hicho wamekuja kuelekezana na mikoa iweze kusomana ili wajue mkoa huu umebajeti kiasi gani ili wote kuongea lugha moja na inakuwa ni rahisi katika utekelezaji wa bajeti yao.

Alisema kama WMA ni wakala ambayo inatakiwa isimamie uzalishaji na matumizi ya vipimo katika viwanda, hivyo sura ya viwanda lazima ionekane katika vipimo.

# 'Wanaokwama elimu wachangiwe mitaani'

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WANANCHI mkoani Kagera wameshauriwa kuanzisha kamati mitaani ambazo zitakuwa na jukumu la kukusanya fedha kwa ajili ya kuwasaidia watoto wanaoshindwa kuendelea na masomo kutokana na kukosa mahitaji ya shuàle.

Akizungumza katika mahafali ya nne na ya sita kwa shule za Kaizilege na Kemebos Manispaa ya Bukoba, Sheikh wa mkoa huo, Haruna Kichwabuta, alisema kama jamii inaweza kuunda kamati za kufanya sherehe kubwa za harusi, kwa nini washindwe kusaidia watoto wenye uhitaji ambao wanakosa haki yao ya kupata elimu kutokana na hali ngumu kiuchumi.

"Mnashindwa kusomesha watoto badala yake mnakimbilia kuwaozesha, mkiona siku ya harusi binti analia mnafurahi na kuimba nyimbo eti harusi imependeza, kumbe yeye analia kwa sababu anawaza namna gani atakabiliana na changamoto za maisha ya huko mnakompeleka bila elimu," alisema Sheikh Kichwabuta.

Alisema tatizo la wazazi kutowasomesha watoto wao lina madhara makubwa ikiwamo kusababisha ongezeko la vitendo vya uhalifu. "Kama kuna watoto wengi ambao hawajasoma fahamu mtaa haukaliki, hata ukiingia msikitini ukaacha viatu nje ukirudi huvikuti, tujitahidi tusomeshe watoto wetu ili kuongeza amani mtaani" alisema.

Aidha, aliziasa shule na vyuo kutoa elimu kwa watoto ambayo itawawezesha baada ya kuhitimu wajiajiri, kuliko kukaa wakisubiri kuajiriwa na kuogeza idadi ya watu wasio na ajira mtaani, huku wakiwa na vyeti vingi vimepambwa kabatini nyumbani.

"Watoto wetu tuwajenge katika misingi ya kumaliza shule ama vyuo wakajiajiri, hii itapunguza kero kwa wazazi badala ya kukuta mzazi analia kwa kufirisika kutokana na kusomesha watoto, lakini hata watoto wanalia wamehitimu hawana ajira" alisema.

Kuhusu elimu bure iliyoanzishwa ili kuhakikisha watoto wote wanakwenda shule hasa wanaotoka katika familia zenye kipato kidogo, alisema ni ajabu sasa awepo mzazi au mlezi asiyetaka kumpeleka mtoto shule wakati serikali imekwishaweka mazingira ya kuwezesha watoto wengi kupata elimu hadi kidato cha nne.

Naye meneja wa shule za Kaizilege na Kemebos, Eurogius Katiti, aliwataka watoto wa kidato cha sita wanaotarajiwa kuanza mitihani yao hivi karibuni kuepuka kujiingiza katika anasa na starehe wawapo nyumbani, na badala yake waendelee kujikita katika masomo kwa manufaa yao ya baadae.

"Wazazi wanajinyima na kujitoa kwa ajili yenu ili mpate elimu, msiwakatishe tamaa wazazi wenu maana mkijiingiza katika starehe mtapotea katika ulimwengu wa maendeleo na kusababisha azma ya wazazi wenu kuwasomesha kutotimia," alisema Katiti.

PSSSF
Public Service
Social Security Fund

Muungano 57



"Tuna kila Sababu ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Letu, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume kwa Misingi Imara na Madhubuti Waliyoiweka Ambayo Imeendelea Kuimarisha Umoja, Amani na Utulivu wa Taifa Letu... Tukiwa Kwenye Muungano Tutafika Mbali Zaidi, na Kufanya Mengi Makubwa Kuliko Tukiwa Mbalimbali".
Rais wa JMT, Mhe.Samia Suluhu Hassan, Oktoba 17, 2020 wakati huo akiwa Makamu wa Rais

Leo. Kesho. Pamoja.
0800 110 055 / 0800110040
www.psssf.go.tz
PSSSFTZ

# Wizara kushirikisha wavuvi kudhibiti uvuvi haramu

**Na Mbaraka Kambona,**
KIGOMA

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo katika mpango wa kuwa na mkakati endelevu wa kudhibiti uvuvi haramu na kuachana na utaratibu wa kuendesha oparesheni za muda mfupi.

Ndaki alisema hayo wakati akizungumza na wavuvi wanaofanya shughuli zao katika Mwalo wa Kibirizi katika Ziwa Tanganyika mkoani Kigoma Aprili 24, 2021.

Ndaki alisema lengo la Wizara ni kuwa na udhibiti wa uvuvi haramu ambao utakuwa endelevu utakaoshirikisha wahusika wenyewe wanaofanya shughuli za uvuvi na viongozi wa eneo husika kuanzia ngazi ya kijiji, kata, wilaya hadi Mkoa.

"Tunataka kuja na mkakati endelevu wa namna ya kudhibiti uvuvi haramu, tuhusike sote, kuanzia wataalamu, viongozi wa ngazi zote na wananchi wanaohusika na uvuvi wenyewe," alisema Ndaki na kuongeza:

"Uvuvi haramu unatishia rasilimali zetu za uvuvi, tusiulee, tuwashirikishe wahusika ili waone kuwa uvuvi haramu ni kitu kisichokubalika."

Kwa mujibu wa Ndaki, walichokigundua katika mkakati wa kutumia oparesheniza muda mfupi ni kwamba matokea yanakuwa ya muda mfupi na operesheni hizo zikiisha matukio ya uvuvi haramu yanaendelea tena kwa sababu operesheni hizo zinahusisha wataalamu kutoka Wizarani na sio wahusika wenyewe wa eneo husika.



Kaimu Mganga Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Jonas Mcharo (aliyeshika mkasi), akizindua kituo cha kisasa cha miundombonu ya kutakasa mikono katika Kituo cha Pamoja cha Huduma za Forodha kilichopo Holili, Wilaya ya Rombo jana. Kimejengwa na Tawasa Net kwa ufadhili wa Shirika la Water Aid Tanzania, kwa gharama ya Sh.mil. 27. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# JKT watengewa ekari 14 kuzalisha vifaranga samaki

**Na Renatha Msungu,**
MLIMBA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limetenga ekari 14 katika Kikosi cha 837 Chita kwa ajili ya uzalishaji wa vifaranga vya samaki kukabiliana na uhaba wa vifaranga nchini na kuboresha ufugaji wa samaki.

Hatua hiyo imechukuliwa ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuzalisha vifaranga vya samaki kwa ajili ya kuboresha ufugaji wa samaki wenye tija nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ziara ya kutembelea kambi ya Kikosi cha 837 Chita iliyoko Mlimba mkoani Morogoro juzi, Mtaalamu wa Samaki katika kikosi hicho, Luteni Joseph Lyakurwa, alisema wameanza utekelezaji wa agizo hilo kwa kujenga matanki ya maji 26 na kuboresha miundombinu.

Alisema shamba hilo la ufugaji samaki kisasa litakuwa kubwa kwa Afrika Mashariki kutokana kwa kuwa litakuwa na uwezo wa kutoa tani 12 kwa mwezi.

Mtaalamu huyo alibainisha kuwa shamba lililopo sasa linatoa tani nne kwa mwezi.

"Tumeanza utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu, tumejenga matanki 26 ya saruji ya kufugia samaki ambayo tunatarajia kuzalisha vifaranga 200,000 kwa mwezi," alisema.

Luteni Lyakurwa alisema vifaranga hivyo vitakidhi mahitaji ya jeshi hilo na kusaidia kukabili uhaba wa vifaranga vya samaki kwa jamii inayofuga.

Alifafanua zaidi kuwa kupitia matanki hayo, kutakuwa na uzalishaji wenye tija kwa maji yanayotoka katika matanki hayo yanakuwa na mbolea.

Luteni Lyakurwa alisema kuwa mbali na ufugaji wa samaki, shamba hilo litatumika kutoa elimu kwa taasisi za vyuo vya elimu ya juu kwa vitendo namna ufugaji wa kisasa unavyokwenda.

"Ukiacha vyuo, taasisi za utafiti zitatumia shamba hilo kufanya utafiti mbalimbali ambao utaleta tija kwa taifa kutokana na matokeo chanya ambayo yatatoka," alisema.

Mtaalamu huyo alibainisha kuwa kwa kuanzia, tayari wana shamba la ekari mbili na nusu ambalo wanalitumia kuzalisha vifaranga bora vya samaki.

Kijana wa Kujitolea katika jeshi hilo, William Lubinza, alisema kupitia mafunzo ya JKT, amejifunza vitu vingi vya kitaalamu ambavyo vitamsaidia pale atakaporejea uraiani.

"Nitawafundisha vijna wenzangu elimu ya kilimo na ujenzi niliyoipata jeshini, ili waondoe dhana ya kuajiriwa badala yake wajiajiri wenyewe," alisema.

# Grand Finale NMB MastaBata yawapa washindi safari za utalii

**Na Beatrice Moses**

WASHINDI 12 wa zawadi kuu 'Grande Finale' ya Kampeni ya NMB MastaBata 'Siyo Kikawaida' wamekabidhiwa zawadi zao mbalimbali, zikiwemo tiketi za ndege tayari kwa safari za utalii wa ndani katika Mbuga za Serengeti, Ngorongoro na Zanzibar.

Hafla ya kukabidhi zawadi na tiketi hizo imefanyika jijini Dar es Salaam, ambako washindi wawili na wenza wao walikabidhiwa tiketi za safari ya utalii katika Hifadhi za Taifa za Serengeti na Ngorongoro, huku wengine 10 wakikabidhiwa zawadi mbadala zenye thamani ya Sh. milioni 7 kila mmoja.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Juma Kimori, alisema Kampeni ya NMB MastaBata iliyozinduliwa Novemba 24, mwaka jana, imemalizika kwa mafanikio makubwa kwa kuongeza idadi ya watumiaji wa kadi na kwamba jumla ya washindi 436 tayari wamekabidhiwa zawadi mbalimbali.

Kimori alibainisha kuwa, miezi mitatu ya kampeni hiyo, ililenga kuhamasisha matumizi ya kadi za MastaerCard QR, MasterPass, Vituo vya Mauzo (PoS) na mifumo mingine ya kidijitali, ambako kulikuwa na mwitikio mkubwa kwa wateja wao.

Aliongeza jumla ya washindi 400 walizawadiwa kiasi cha Sh. 100,000 kila mmoja, huku wengine 20 wakijinyakulia zawadi za simu janja aina ya Samsung Note 20 zenye thamani ya Sh. milioni 2.4 (kila moja), wakati washindi wa Grande Finale wakijinyakulia zawadi za Sh. milioni 7 kila mmoja. Mpaka kufikia mwisho, benki ya NMB imetumia shilingi milioni 200 kufanikisha promosheni hiyo

Alizitaja zawadi za washindi wa Grande Finale kuwa ni friji kuwa la milango miwili, televisheni kubwa ya Samsung (inchi 55) iliyolipiwa king'amuzi cha DSTv kwa miezi mitatu, microwave, water dispenser kompyuta mpakato 'laptop' na simu ndogo ya Samsung.

Kwa upande wake, Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, aliwapongeza washindi wa MastaBata waliotoka katika Kanda yake na Tanzania nzima kwa ujumla na kwamba huduma za matumizi kwa kadi unaendelea kupitia Pay E na MastaBata.

Akizungumza kwa niaba ya washindi wengine, Ali Aboubakar Ali, ambaye alichagua zawadi mbadala ya vitu badala ya safari ya utalii, alisema ushindi alioupata kumuwezesha kutwaa zawadi hizo, unathibitisha namna droo za kampeni hizo zilivyozingatia bahati za washiriki.

Nipashe
Spotika



NYAKATI 10 MAARUFU ZA RONALDO KATIKA SOKA UK. 12-13



# MAMBO MATANO YALIYOANGUSHA MASHINDANO MAPYA ULAYA (ESL)

## ISIKUPITE

KATIKA karne hii ya 21, kombinesheni ya washambuliaji wawili inayoongoza kwa kufunga mabao mengi zaidi hadi sasa ni ya Luis Suarez (mabao 59) na Lionel Messi (mabao 41), kwa pamoja wakifunga jumla ya mabao 100 wakati wakiitumikia Barcelona msimu wa 2015-16.



**NYON,** Uswisi

BAADA ya maandamano makali kutoka kwa mashabiki, klabu za soka zilizojiunga na mashindano mapya ya Klabu barani Ulaya (European Super League) zikaamua kujiondoka kwenye mashindano hayo yenye utata. Hata hivyo, inabakia kuona ni mabadiliko gani yatakayofanywa kwa klabu hizo 12.

Sifa kubwa wanatakiwa kupewa mashabiki, huku pia mtazamo utabakia kwa wamiliki wa klabu hizo ambao waliamua kujiunga na ESL.

Wamiliki kama wa Arsenal, Stan Kroenke, Manchester United, Glazers na John Henry wa Liverpool wapo kwenye wakati mgumu.

Makala hii inaangalia mambo matano yaliyochangia kuangushwa kwa mashindano hayo mapya ya Ulaya.

### #5 VITA NA MASHIRIKISHO YA SOKA

Anguko lilianza mara tu baada ya kutangazwa kwa mashindano hayo. Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya, UEFA, lilikasirika, na rais wake, Aleksander Ceferin aliweka wazi mashaka yake juu ya mashindano hayo.

EFL pia ilitoa taarifa yenye nguvu ya kupinga mashindano hayo na ripoti ilisema kwamba, klabu zilizohusika kwenye mashindano hayo, zingetolewa kwenye Ligi zao za nyumbani.

Hata Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, alielezea kusikitishwa kwake, akionyesha ukali kuhusu hali hiyo. Shinikizo hilo lote lilionekana kufanya kazi.

### #4 KAULI ZA KLABU ZILIZOKUWA NJE YA SUPER LEAGUE

Hasira zilionyeshwa na klabu kadhaa ambazo hazikujumuishwa kwenye ligi hiyo, huku kwenye mitandao ya kijamii kukijaa kauli za kulaani.

Hata Wolverhampton Wanderers ikajitangza yenyewe kuwa ndio bingwa wa Ligi Kuu England msimu wa 2018/19, kwa sababu ilimaliza nafasi ya saba, nyuma ya zile sita zilizojiunga na European Super League.

Klabu kadhaa zilitoa taarifa zake kulaani kuanzishwa kwa mashindano hayo.

Kulikuwa na ripoti kwamba, klabu zote zilizokuwa nje ya ESL zilitaka timu zilizojiunga na ligi hiyo mpya kuondolewa kwenye ligi zao za nyumbani.

### #3 MATENDO YA WACHEZAJI

Mchezaji wa Paris Saint-Germain, Ander Herrera alichapisha barua ya kusisimua kulaani kuundwa kwa mashindano hayo, na wachezaji wengi wa sasa na zamani walifanya hivyo.

Wachezaji wa Manchester United, Marcus Rashford, Luke Shaw na Bruno Fernandes walionyesha wazi hisia zao, huku hotuba ya Gary Neville ilitazamwa sana. Nahodha wa Liverpool, Jordan Henderson aliitisha mkutano kwa manahodha wote wa Ligi Kuu England na akachapisha maoni yake kwenye mtandao wa kijamii.

Mchezaji wa Everton, Richarlison, Daniel Podence wa Wolverhampton Wanderers na mlinzi wa kati wa zamani wa Liverpool, Dejan Lovren, mlinzi wa kushoto wa Atalanta, Robin Gosens na mchezaji wa zamani wa Arsenal na Real Madrid, Mesut Ozil wote walizungumza kuhusu kutofurahishwa kwao na mashindano hayo.

### #2 MAHOJIANO YA FLORENTINO PEREZ

Rais wa Real Madrid na Mwenyekiti wa ESL, Florentino Perez alifanya mahojiano yenye utata na El Chiringuito, ambayo yalizidisha msuguano mkali kati ya mashabiki na wamiliki wa klabu.

Perez alisema mashabiki wenye umri wa miaka 16 hadi 24 hawakuwa na mapenzi na mpira wa miguu na alipendekeza kupunguzwa kwa dakika kwenye soka ndio inaweza kuwa suluhisho. Hilo lilikutana na upinzani na ukosoaji mkubwa.

Pia alisema klabu zimepoteza fedha nyingi katika misimu ya hivi karibuni na, ESL ndio ilikuwa njia sahihi ya kwenda kujikwamua. Mahojiano hayo ya Perez yaliongeza kasi ya maandamano, na mashabiki wakapaza sauti zao kwa hasira kwenye mitandao ya kijamii.

### #1 MANDAMANO YA MASHABIKI

Jambo moja ambalo limesababisha kiukweli kuanguka kwa mashindano hayo ni maandamano ya mashabiki.

Mashabiki waliingia barabarani kupinga kuundwa kwa mashindano hayo mapya ya Ulaya. Mechi ya Liverpool na Leeds United ilishuhudia mashabiki wakijaribu kuzuia basi la wekundu hao kuingia pale kwenye dimba la Elland Road. Mashabiki wa Chelsea walifanya jukumu lao pia, wakamlazimu Petr Cech kuwatuliza nje ya Uwanja wa Stamford Bridge.

Kandanda ni mchezo kwa mashabiki. Umoja ulioonyeshwa dhidi ya uchoyo wa wamiliki wa klabu utatumika kama onyo kwa wamiliki wa klabu kabla ya jaribio lingine lolote.

# NYAKATI 10 MAARUFU ZA RONALDO KATIKA SOKA




**LISBON,** Ureno

CRISTIANO Ronaldo ni mmoja wa wachezaji wakubwa waliopamba mchezo huo. Licha ya kutimiza miaka 36 mwaka huu, Ronaldo haonyeshi dalili zozote za kusimama wakati wowote hivi karibuni, kwani anaendelea kuwa mchezaji bora wa klabu na nchi yake.

Kwa kipnindi cha karibu miongo mwili ya kucheza soka, raia huo wa Ureno amefunga mabao mengi na kushinda tuzo nyingi. Kuzitaja kwa uchache, mshindi mara tano wa Ballon d'Or na mfungaji bora wa muda wote wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Ureno.

**Akiwa hodari hewani na akicheza kwa miguu yote miwili Ronaldo anapenda kucheza soka, mchezo anaoupenda zaidi.**

### #1 'ILE' KELELE DHIDI YA PORTO (2009)

Akicheza msimu wake wa sita kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ronaldo alikuwa na mabao 12 katika michezo 49 kuelekea robo fainali ya msimu wa 2008-09 kule Porto.

Baada ya mchezo wa kwanza pale Manchester United kumalizika kwa sare ya 2-2, Porto walikuwa na faida kwenye mchezo wa pili shukrani kwa mabao mawili waliyoyapata kule Old Trafford. Hata hivyo, Ronaldo alikuwa na mawazo mengine.

Dakika sita tu ya mchezo huo, Ronaldo alipokea mpira katikati ya uwanja na akaruka na akiwa umbali wa yadi 40 na kupika kelele na mpira ukaenda kujaa kona ya chini kwenye nyavu za goli la Porto.

Ronaldo baadaye akaliita 'bao bora' zaidi kwa aliyowahi kufunga kwa wakati ule.

Bila shaka, alifunga mabao mengi mazuri tangu hapo, lakini lile dhidi ya Porto linabakia kuwa kitu fulani maalumu kwake.

### #2 MCHEZAJI WA KWANZA KUFUNGA TIMU MBILI TOFAUTI FAINALI YA LIGI YA MABINGWA (2014)

Miaka sita baada ya kuifungia Manchester United kwenye ushindi dhidi ya Chelsea kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2008, Ronaldo alikuwa kwenye mchezo huo tena, wakati huu akiwa na timu tofauti.

Katika fainali ya kwanza iliyozikutanisha timu zote kutoka nchini Hispania kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kule Lisbon mwaka 2014, Ronaldo alikuwa mmoja wa wafungaji watatu wa Real Madrid baada ya muda wa ziada kwa Los Blancos hao kuwafunga Atletico Madrid na kushinda taji hilo.

Na hiyo ikamfanya Ronaldo kuwa mchezaji pekee kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kufunga kwenye fainali kwa timu mbili tofauti zilizotwaa ubingwa.

### #3 MFUNGAJI BORA WA MUDA WOTE WA REAL MADRID (2015)

Miaka sita baada ya kutua Real Madrid, Ronaldo alifunga dhidi ya Levante katika mchezo wa LaLiga msimu wa 2015-16 na kuipiku rekodi ya Raul (323) na kuwa mfungaji wa wakati wote wa klabu hiyo kwenye mashindano yote.

Katika kipindi hicho, Ronaldo alifunga mabao 50 ndani ya misimu mitano; mabao 61 ndio yakiwa mengi zaidi kwa msimu wa 2014-15.

Wakati akiondoka Real Madrid kwenda Juventus kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2018, Ronaldo alikuwa amefunga mabao 450 katika mechi 438, akishinda mataji 16.

### #4 ANASHINDA TAJI LA ULAYA NA URENO (2016)

Miaka 12 baada ya kukosa mashindano ya Ulaya akiwa kijana, wakati Ureno ilipofungwa na Ugiriki isiyofungika kwenye fainali nyumbani, Ronaldo alishinda taji la mashindano hayo kwa kuifunga Ufaransa katika fainali ya mwaka 2016 jijini Paris.

Mapema katika mashindano hayo Ronaldo alikosa penalti dhidi ya Austria lakini alifunga mara mbili kwenye sare ya 3-3 dhidi ya Hungary. Pia alifunga kwenye ushindi wa 2-0 dhidi ya Wales kwenye nusu fainali, huku pia akitoa pasi ya mwisho kwenye raundi ya 16 kwenye muda wa ziada dhidi ya Croatia na kufunga penalti dhidi ya Poland.

Katika mechi yake kubwa zaidi ya kimataifa, Ronaldo alidumu kwa dakika thelathini tu uwanjani, wakati Dmitri Payet akimjeruhi goti lake la kushoto. Ronaldo aliyekuwa analia machozi alijaribu mara mbili kuungana tena na hatua hiyo na goti lililofungwa sana kabla ya kuondoka uwanjani.

Karibu saa moja baadaye, Ronaldo alilia kwa mara ya tatu usiku huo, wakati huu akimwaga machozi ya furaha, wakati Ureno ilipopata ushindi wa bao 1-0 kwenye muda wa ziada dhidi ya Ufaransa na kuwa mabingwa wapya wa Ulaya.

### #5 MCHEZAJI WA KWANZA KUFUNGA MABAO 100 KWENYE LIGI YA MABINGWA ULAYA (2017)

Baada ya kuanza taratibu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ronaldo ilimchukua mechi 27 kufungua akaunti yake kwenye mashindano hayo - na hasa baada ya kujiunga na Real Madrid.

Ronaldo alifunga kwa misimu saba mfululizo angalau kwa mabao kumi, sita kati yake ikamfanya kufikisha mabao 100 kwenye historia ya mashindano hayo. Ronaldo alifunga hat-trick, dhidi ya Atletico Madrid kwenye nusu fainali kabla ya kufunga mara mbili dhidi ya Juventus - klabu yake ya sasa - kwenye fainali na kushinda taji lake la nne kwenye mashindano hayo.

### #6 'LILE' GOLI DHIDI YA JUVENTUS (2018)

Ronaldo bila shaka alifunga moja ya bao bora zaidi kwenye historia ya mashindano hayo kwenye mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Real Madrid dhidi ya Juventus.

Ronaldo alikutana na krosi na kuruka juu futi moja na kupiga mpira kwa kichwa ambao ulimshinda golikipa, Gianluigi Buffon.

Real Madrid waliondoka na ushindi wa 3-0 usiku huo kabla ya penalti ya Ronaldo kwenye mchezo wa pili kuwawezesha Blancos hao kupata ushindi wa uwiano wa mabao 4-3.

### # 7 MATAJI MATANO YA LIGI YA MABINGWA ULAYA (2018)

Bila shaka alikuwa akifurahi wakati bora zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2017-18, Ronaldo alikuwa mchezaji wa kwanza kufunga katika mechi zote sita za hatua ya makundi.

Akaendelea kufunga zaidi katika mechi nne zilizofuata, akifunga kwenye mechi zote mbili za ushindi za Real Madrid hatua ya 16 na robo fainali. Baadaye akafunga dhidi ya Juventus, ambayo alijiunga nayo.

Wakati Real Madrid wakiifunga Liverpool 3-1 kwenye fainali, Ronaldo akawa mchezaji wa kwanza kushinda mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu kuundwa upya kwa mashindano hayo mwaka 1992.

### #8 HAT-TRICK YA KUKUMBUKWA KOMBE LA DUNIA DHIDI YA HISPANIA (2018)

Ronaldo alianza mashindano ya Kombe la Dunia mwaka 2018 nchini Urusi kwa kishindo. Hat-trick yake nzuri iliisaidia Ureno kupata sare ya 3-3 dhidi ya mabingwa wa zamani wa mashindano hayo, Hispania kwenye mchezo wao wa ufunguzi.

Penalti ya Ronaldo iliwawezesha Ureno kupata uongozi kabla ya kuiweka tena mbele baada ya Hispania kusawazisha kabla ya mapumziko.

Wakati Hispania ikifunga mara mbili kipindi cha pili Ronaldo akasawazisha kwa shuti la adhabu ndogo.

Mapema kwenye mchezo huo, bao lake la kwanza lilimfanya Ronaldo kuwa mchezaji pekee kufunga mara nane mfululizo kwenye mashindano makubwa. Bahati mbaya, ulikuwa mchezo wa kwanza kati ya 51, ambapo timu ya Ronaldo haikushinda licha ya hat-trick yake.

### #9 HAT-TRICK YA KWANZA KWA JUVENTUS ILIYOSUBIRIWA SANA (2019)

Ronaldo alitimiza ahadi yake ndefu ya kufunga mara tatu kwenye mchezo huo, wakati akifunga hat-trick yake ya pili kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atletico Madrid.

Alisaidia Juventus kupindua matokeo ya 2-0 kwenye mchezo wa kwanza na kupata ushindi wa 3-2 kwenye mchezo wa pili na kutinga robo fainali msimu wa 2018-19.

Mabao hayo pia yalimsaidia Ronaldo kufunga hat-trick yake ya kwanza akiwa kwenye jezi ya Bianconeri hao.

### #10 MCHEZAJI WA KWANZA ULAYA KUFUNGA MABAO 100 YA KIMATAIFA

Akiendelea kunga'ra kwenye mwanzo wa msimu wa 2020-21, licha ya wiki chache za mlipuko wa virusi vya corona, Ronaldo alifunga dhidi ya Sweden kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa na kuwa mchezaji wa kwanza wa Ulaya kufunga mabao 100 ya kimataifa.

Akicheza mchezo wake wa 165 katika jezi za Ureno, Ronaldo alifunga bao la kwanza kwa shuti la adhabu ndogo. Akafunga la pili na kuisaidia Ureno kushinda 2-0.

Mabao 102 ya Ronaldo sasa yanamfanya kupitwa saba tu na gwiji wa Iran, Ali Daie mwenye mabao 109 kwenye mechi za kimataifa.

## Nukuu

"Kuna mechi nyingi, lakini timu itakayokwenda kushinda itahitaji kupata ushindi kwa mechi zake zote na sisi tutafanya kila tunaloweza, hasa kwa wachezaji wangu. Tunatakiwa kuwa kwenye ubora wetu, hatuna namna nyingine, kwani tukitaka kushinda taji hili lazima tushinde kila mchezo uliopo mbele yetu," **Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane, akizungumzia mbio za ubingwa wa LaLiga.**



"Nahisi Paul ni miongoni mwa wachezaji bora duniani kwa sasa, na huwa anatoa ushauri kwa wenzake kwenye vyumba vya kubadilishia nguo. Kwangu mimi, kucheza na Paul kunanifanya nionyeshe uwezo mkubwa. Kucheza na mtu anayejua kunanifanya nifanye mazuri zaidi na nahisi hilo limenifanya kuonyesha uwezo mkubwa sana tunapokuwa uwanjani," **Kiungo wa Manchester United, Bruno Fernandes.**



"Christiano Ronaldo hatokuja tena Real Madrid. Haileti maana yoyote, ana mkataba na Juventus. Nampenda sana ametupa vitu vingi. Hatujafanya mazungumzo yoyote naye wala Juventus, na kwa uhakika kabisa hakuna mpango wa kumrejesha hapa Ronaldo, yeye ni mchezaji wa Juventus kwa sasa na ana mkataba kule," **Rais Klabu ya Real Madrid, Florentino Perez.**





# VITA YA KUEPUKA KUSHUKA DARAJA VPL MSHIKEMSHIKE

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikielekea ukingoni na timu za Simba, Yanga na Azam FC zikipigana kusaka ubingwa, zipo klabu ambazo kwa sasa zinapigana vikumbo kuepuka kukaa kwenye sehemu mbaya inayoweza kusababisha kushuka daraja.

**Jumla ya timu nne za mwisho zinatarajia kushuka daraja moja kwa moja, na mbili za juu zitakwenda kucheza mechi za mtoano ambazo ndizo zitaamua hatima yao kama zitabaki au zitashuka daraja endapo zitafungwa michezo hiyo ya mwisho.**

Msimu huu kuna timu 18, hivyo timu iliyoshika nafasi hiyo hadi ya 15 zote zitashuka moja kwa moja. Itakayoshika nafasi ya 14 wakati ligi itakapomalizika na ya 13, ndizo zitakazoenda kwenye mtoano.

Timu hizo mbili zitakwenda kucheza na timu zilizokamata nafasi ya pili kwenye Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara kwenye makundi A na B.

Mwandishi wa makala haya, anaziangalia timu ambazo ziko hoi bin taaban, zikipigania uhai wao wa kubakia katika ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**1. MWADUI FC-POINTI 16**

Ni miujiza pekee ambayo inaweza kuifanya timu hii isishuke daraja, au isiwe ndani ya timu zitakazokwenda kucheza mechi za mchujo maarufu kama 'play off'.

Tangu ligi inaanza imekuwa kwenye eneo la hatari na pamoja na kucheza mechi 27 mpaka sasa, ina pointi 16 tu. Imeshinda mechi nne, sare nne na kufungwa mechi 19. Imebakisha mechi saba tu.

Mwadui ni timu ambayo hata msimu uliopita ilibahatika kutoshuka daraja kwenye mechi ya mwisho.

Mbali na kuburuza mkia, ndiyo timu iliyoweka rekodi ya kufungwa mabao mengi msimu huu. Imetandikwa mabao 52 mpaka sasa.

**2. IHEFU SC-POINTI 27**

Pamoja na kujitutumua siku za karibuni, lakini timu ya Ihefu yenye maskani yake Mbarali jijini Mbeya ambayo imeanza kucheza Ligi Kuu msimu huu, ipo kwenye hatari ya kushuka daraja.

Kabla ya mechi ya jana dhidi ya Coastal Union, ilikuwa kwenye nafasi ya 17, ikiwa na pointi 27 kwa michezo 27.

Ihefu ambayo mzunguko wa pili imeonekana kuimarika, iliathiriwa zaidi na mechi zake za mzunguko wa kwanza ilipoonekana kuwatumia zaidi wachezaji iliotoka nao Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Ilifanya usajili kipindi cha dirisha dogo kuongeza baadhi ya wachezaji wazoefu akiwemo kipa, Deogratius Munishi 'Dida' ambao wameifanya angalau kuwa bora chini ya kocha wa zamani wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila.

Tatizo ni kwamba ni kama ilichelewa, kwani timu nyingi sasa zimeamka na kupigana ili zisishuke.

**3. MBEYA CITY-POINTI 27**

Ni timu nyingine ya Mbeya ambayo nayo ipo kwenye hatari ya kushuka daraja pia.

Mbeya City imeonekana kama vile haikujifunza kilichoipata msimu uliopita, ilipolazimika kurejea Ligi Kuu kwa mlango wa nyuma, ilipoifunga Geita Gold kwenye mechi ya 'play off', vinginevyo saa hizi ingekuwa ni historia.

Kama Ihefu vile, Mbeya City nayo imecheza mechi 27 na kujikusanyia pointi 27. Mechi saba ilizobakisha ndizo zitaamua kama kushuka, kucheza 'play off', au kuepuka kushuka.

**4. KAGERA SUGAR-POINTI 27**

Kagera Sugar kwa miaka ya karibuni imeonekana kama kupungua nguvu. Itakumbukwa kuwa msimu wa 2018/19 nusura ishuke daraja baada ya kutokea hitilafu ya takwimu kwenye Bodi ya Ligi.

Timu hiyo ilikwenda kucheza mechi ya 'play off', dhidi ya Pamba ya jijini Mwanza na kurejea Ligi Kuu. Inashika nafasi ya 15, ikiwa na pointi 27, baada ya kushuka dimbani katika michezo 27.

Kwa mechi saba zilizosalia, inaweza kuepuka kushuka daraja, kushuka au kwenda kucheza 'play off' kama ilivyowahi kufanya misimu miwili iliyopita.

**5. JKT TANZANIA-POINTI 27**

Maafande wa JKT Tanzania msimu huu hawako vizuri sana. Wana pointi 27 na kuwa kwenye eneo ambalo si salama. Ila yenyewe imecheza mechi 26 tofauti na timu nyingine zenye pointi 27.

Inashika nafasi ya 14 na mechi nane ilizobakisha ndizo zitaamua mustakabali wa kubaki au kushuka daraja. JKT Tanzania ni timu ya muda mrefu kwenye Ligi Kuu, tangu ilipokuwa inaitwa JKT Ruvu.

**6. MTIBWA SUGAR-POINTI 28**

Ni timu pekee inayopigania kushuka daraja ambayo imeshawahi kuwa bingwa wa Tanzania Bara mwaka 1999 na 2000.

Ilikuwa ni timu ya kutisha miaka mingi iliyopita. Kwa miaka ya karibuni imeonekana kupoteza mvuto. Inashika nafasi ya 13 ikiwa na pointi 28, ambazo bado hazijaihakikishia kubaki Ligi Kuu.

Msimu uliopota iliponea chupuchupu kwenye mechi ya mwisho, ilipoifunga Ruvu Shooting mabao 2-1.

**JE, WAJUA?**



SHEIKHE Mansour wa Manchester City, ndiye tajiri zaidi kuliko wamiliki wote wa klabu akiwa na utajiri wa dola bilioni 30, akifuatiwa na mmiliki wa RB Leipzig/ Red Bull Salzburg, Dietrich Mateschitz ambaye ana utajiri wa dola bilioni 26.9.





Sehemu ya wavuvi wanaofanya shughuli zao katika Mwalo wa Kibirizi wakifuatilia matukio yanayoendelea katika mkutano wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (hayupo pichani), uliofanyika mkoani Kigoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jafo awabana wakurugenzi ujenzi madampo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amewaagiza wakurugenzi wa halmashauri za majiji na miji ambayo serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa madampo ya kisasa, kuimarisha usimamizi ili kulinda afya za wananchi.

Jafo alitoa agizo hilo jana jijini Dodoma alipozuru kukagua shughuli zinazofanywa katika dampo la kisasa la Chidaya, nje kidogo ya Jiji la Dodoma. Alisema licha ya serikali kutumia kiasi kikubwa cha fedha katika utekelezaji wa miradi hiyo, pamekuwa na udhaifu katika usimamizi, hali inayotishia afya za wananchi katika maeneo hayo.

Jafo alisema usimamizi wa jiji katika dampo la kisasa la Chidaya unahitajika ili kusaidia kuimarisha afya za wananchi wanaoishi katika maeneo jirani.

"Ninatoa mwezi mmoja kwa Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma kuhakikisha haya mabwawa ambayo yanahifadhi maji taka yatokanayo na takataka zinazoletwa hapa, mjenge ukuta ili kulinda yasivuje kwenda katika mito ya jirani hali inayoweza kuleta madhara kwa wananchi wetu," aliagiza.

Waziri huyo alisema maji hayo yatokanayo na uchafu yanaweza kuwa na kiwango fulani cha sumu ambacho kama hakitadhibitiwa vizuri na kuingia katika vyanzo vingine vya maji, kitakua hatari kwa maisha ya wananchi.

"Ninaagiza myapime haya maji ili kubaini kiasi gani cha sumu kipo ndani na baadaye myatibu. Lakini pia suala la kujenga ukuta kulinda haya maji ni la muhimu sana ili yasije kwenda katika vyanzo vingine vya maji na watu wakayatumia kwa kunywa," alisema.

Jafo alisema halitakuwa jambo la busara kwa viongozi wa jiji kuacha maji hayo yenye sumu kusambaa kwenda katika maeneo mengine ambayo yanaweza kuleta madhara makubwa.

"Hapa kuna mto mmeniambia unapita jirani, sasa mhakikishe maji haya yanadhibitiwa ili yasije kuingia kule na wananchi kwenda kuyatumia yakaleta madhara makubwa," aliagiza.

Katika hatua nyingine, Waziri Jafo alizindua Baraza la Kazi la Wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Rais huku akiwataka watumishi kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Alisema watumishi wa umma watakiwa kufanya kazi kwa jitihada ili kuacha alama katika utumishi wao na siyo vinginevyo.

"Tuache kufanya kazi kwa mazoea, kila mmoja wetu atimize wajibu wake ili tuache alama. Leo hii katika ofisi zetu kuna watu hata akisafiri, hakuna anayehisi pengo lake, hii yote ni kutokana na kuwa hatujafanya kazi za kututambulisha uwapo wetu," alionya.

# TALIRI yapewa jukumu kuongeza tija ya mifugo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, ameiagiza Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kufanya utafiti utakaolisaidia taifa kupiga hatua kupitia Sekta ya Mifugo.

Prof. Ole Gabriel aliagiza hayo jana jijini Dodoma alipozungumza kwenye kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa taasisi hiyo.

Alisema hakuna taasisi nyingine ambayo wizara hiyo inaitegemea katika utafiti zaidi ya TALIRI, hivyo ni lazima ifanye utafiti utakaoboresha sekta hiyo na kuchangia pato la taifa.

"Tusibakie kujisifu tu kuwa Tanzania ni nchi ya pili barani Afrika kwa idadi kubwa ya mifugo. Lazima tujisifie kwa namna tutavyoweza kutumia sekta hii kukuza uchumi wa taifa," aliagiza.

Alisema kuwa utafiti ndiyo utakaosaidia taifa kupiga hatua kufikia nchi ambazo zimefanikiwa katika sekta hiyo. "Kama Rais (Samia Suluhu Hassan) alivyokuwa akitoa hotuba yake bungeni, alisema ng'ombe wetu akichinjwa nyama yake haiwezi kuzidi kilo 150. Hii yote ni kutokana na kutokuwa na utafiti wa mbegu bora ambazo zitaweza kutoa kiasi cha kutosha cha nyama," alisema.

Alisema TALIRI pia inatakiwa kufanya utafiti wa mbegu bora za ng'ombe ili kuwa na uhakika wa nyama ya kutosha pamoja na maziwa. "Lazima sekta hii ya mifugo tuihuishe na Tanzania ya viwanda, hivyo basi tunatakiwa kuhakikisha ng'ombe wetu wanatoa nyama ya kutosha na iliyo bora, maziwa mengi, ngozi pamoja na pembe na kwato," alisema.

Mtendaji huyo wa wizara alisema sekta hiyo ikishindwa kuwa na bidhaa zitokanazo na mazao ya mifugo bora, hata malighafi kwa ajili ya viwanda hazitakidhi viwango.

Aliiagiza TALIRI kuhakikisha inakuwa na ubunifu katika kuangalia vikwazo vipya vinavyohusu wafugaji na nchi ili kuzifanyia kazi mara moja.

Mwenyekiti wa Baraza hilo na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TALIRI, Dk. Jonas Kizima, alisema kikao hicho ni cha pili kwa baraza hilo na moja ya kazi yake ni kupitia bajeti yake.

# Waziri Mkumbo ashiriki mkutano dharura EAC

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

TANZANIA imeshiriki katika mkutano wa 37 wa dharura wa Baraza la Mawaziri kwa sekta za biashara, viwanda, fedha na uwekezaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Katika mkutano huo ulifanyika mwishoni mwa wiki kwa njia ya mtandao ukiwa na ajenda ya kujadili uendelezaji wa sekta hizo katika jumuiya hiyo, ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo na Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya.

Prof.Mkumbo alisema jana kuwa mkutano huo ulilenga kujadili uendelezaji wa sekta ya viwanda katika jumuiya hiyo kwa kuzingatia maelekezo yaliyopita ya wakuu wa nchi na Baraza la Mawaziri la jumuiya.

Mbali na Tanzania, mkutano huo pia uliwahusisha wanachama wa jumuiya hiyo ambao ni Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, na Sudani Kusini, ukiwa chini ya uenyekiti wa Jamhuri ya Kenya na Katibu wa mkutano huo alitoka Burundi.

Kwa Tanzania mbali na mawaziri hao wawili, maofisa waandamizi kutoka Wizara za Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara Madini.

Awali, mkutano huo ulitanguliwa na mkutano wa ngazi ya watendaji wakuu wa EAC katika sekta hizo uliofanyika kwa njia ya mtandao, ukiongozwa na Wizara ya Viwanda na Biashara na kwa Tanzania ulihudhuriwa na wataalamu kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Madini.

Wengine ni kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Shirika la Viwango (TBS), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO), Chama cha Wazalishaji Nguo na Bidhaa za Nguo Tanzania (TEGAMAT) na Mfamasia Mkuu wa Serikali.





# Makandarasi waahidiwa neema

**Na Joseph Mwendapole,**
MBEYA

SERIKALI imeahidi kuendelea kutenga miradi ya ujenzi kwa ajili ya kuwaendeleza makandarasi wazalendo, lakini imewaonya kuacha kujihusisha na vitendo vya rushwa kwenye kuomba zabuni.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Leonard Chamuriho, wakati akifunga mafunzo ya siku mbili kwa makandarasi zaidi ya 300 wazalendo wa nyanda za juu kusini uliofanyika jijini Mbeya.

Waziri alisema serikali inatamani ufike wakati kazi za miradi mikubwa iwe inafanywa na makandarasi wazalendo na kuisifu Bodi ya Makandarasi (CRB) kuwa imekuwa ikiwaandalia mafunzo ya mara kwa mara.

Chamuriho alisema iwapo hilo litawezekana fedha nyingi zinazokwenda nje hivi sasa kutokana na kazi za fedha nyingi kufanywa na makandarasi wageni zitabaki hapahapa na kusaidia shughuli za uchumi.

"Napenda kuipongeza bodi ya CRB kwa kweli kazi hii wameifanya kwa ufanisi mkubwa kwani wamekuwa wakiaanda mikutano kama hii ya wadau kila mwaka na nimeambiwa bado mingine kama hii mitatu ya Arusha Dar es Salaam na Mwanza, serikali itafuatilia na kuchukua mapendekezo yenu na kuyafanyia kazi," alisema Waziri Chamuriho.

Alisema serikali haifurahii kuona miradi mikubwa ya kimkakati kama ujenzi wa reli ya kisasa SGR na mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere Rufiji kwani zikifanywa na makandarasi wa ndani serikali itaokoa fedha nyingi na kufanya shughili zingine

Alisema katika mkakati huo wa kuwainua wazalendo, serikali itasimamia sheria ya manunuzi kuhakikisha miradi yote isiyozidi milioni 10 wanapewa makandarasi wa ndani kwani fursa hiyo iko kisheria na inahitaji utekelezaji pekee.



Mwenyekiti wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Injinia Consolatha Ngimbwa akimsindikiza Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho mara baada ya kufunga mkutano wa siku mbilli wa mashauriano na makandarasi zaidi ya 300 wa nyanda za juu kusini ulioandaliwa na bodi hiyo mwishoni mwa wiki jijini Mbeya. **PICHA NA JOSEPH MWENDAPOLE**

Waziri aliwataka makandarasi hao wanapopewa kazi za ujenzi kuhakikisha thamani ya fedha inaonekana na miradi ikamilike kwa wakati na kwa kuzingatia makubaliano ya kwenye mikataba yao. Mwenyekiti wa bodi ya CRB, Consolatha Ngimbwa, alisema utaratibu wa serikali kutumia force account kujenga miradi yake umekuwa ukiwaumiza makandarasi hivyo kushindwa kuongeza mitaji.

Alisema baada ya makandarasi kulalamikiwa kwamba zabuni zao ziko juu na hawajui kujaza zabuni hizo, CRB iliamua kufanya mafunzo nchi nzima kwa makandarasi hao na sasa wameshaiva na wako mahiri kwenye ujazaji wa zabuni hizo. "Mheshimiwa Waziri kwa sasa tulipofikia kunatia matumaini na tunaomba mtupe kazi yoyote tutaifanya kwa ufanisi na kwa wakati kwasababu makandarasi hawa tuliwapa mafunzo na wameiva," alisisitiza Mhandisi Consolatha Ngimbwa.

Aliwaka makandarasi kuungana ili waweze kuwa na mitaji mikubwa na zana za kazi hali ambayo itawawezesha kumudu kutekeleza miradi mikubwa na kuacha ubinafsi wa kila mtu kufanyakazi kifyake vyake.

Alisema kuna baadhi ya makandarasi ambao walijaribu kufanya miradi ya ujenzi pamoja lakini wengi wamekuwa wakianza vizuri na kumaliza vibaya kutokana na ubinafsi wa baadhi yao.

Alisema makandarasi hao kwenye maazimio yao wanataka kuanzisha benki itakayowasaidia kuwakopesha wanapokwama kwenye kutekeleza miradi lakini hawawezi kufanikiwa bila kuungana na kuwa na sauti moja ya kuwasemea.

"Tuna vyama vingi vya makandarasi lakini nashauri ikiwezekana tuviunganishe tuwe na chama kimoja chenye nguvu ili kupata sauti ya kuzungumza na serikali kuhusu changamoto zetu....hata hii benki tunayosema leo hatuwezi kuianzisha bila kuwa kitu kimoja maana tutashindwa kuiendesha," alisema

## Wenye ujuzi ujenzi wa vyoo wapigiwa debe la mikopo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, Wiliam Ntinika, amezishauri Wilaya zote za Mkoa wa Mbeya kuwa asilimia 10 ya fedha za Halmashauri zilizotengwa kwa ajili kuviwezesha vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu, ziwanufaishe pia vijana wenye ujuzi wa ujenzi wa vyoo bora.

Ntinika aliyasema hayo jana wakati wa kuhitimisha mradi wa kuwajengea uwezo vijana wa Halmashauri tatu ikiwemo Mbarali, Chunya na Mbeya, namna ya kutumia ujuzi wa kujenga vyoo bora kibiashara.

Alisema Halmashauri zitoa kipaumbele kwa vijana 121 waliopata elimu ya ujenzi wa vyoo bora baada ya kupata ufadhili na Shirika lisilokuwa la kiserikali la Catholic Relief Services (CRS) kwa kushirikiana na Human Development Innovation Fund (HDIF) kugharamia mafunzo ya Ufundi Veta ili kujenga vyoo vilivyokidhi vigezo.

"Vijana hawa wapewe mikopo ya vifaa vya ujenzi ili wafanye kazi zao bila vikwazo vyovyote, tuendelee kuwahamasisha waliopata ujuzi huo wajiunge kwenye vikundi ili wanufaike na maofisa maenedeleo wawatambue," alisema Ntinika.

Aidha, alilipongeza Shirika la CRS kwa kushirikiana HDIF kuwasaidia vijana ambao hawakuwa na ujuzi wowote wa biashara kuwapa maarifa ya namna ya kujenga vyoo bora kupitia mafunzo ya VETA pamoja na kupewa elimu ya ujasirimali ili kujikwamua kiuchumi.

Mshauri wa Ufundi wa Shirika la CRS, Mhandisi, Godfrey Mpangala, alisema mradi huo wa miaka mitatu umekuwa chachu ya kuleta mabadiliko kwa jamii hasa matumizi ya vyoo bora.

Alisema vijana 124 kutoka Wilaya za Chunya, Mbarali na Mbeya wameisaidia jamii kutambua umuhimu wa kujenga vyoo bora vilivyokidhi vigezo ambapo kupitia ujuzi wao wamejenga kwa gharama nafuu.

Meneja Mradi wa HDIF, Evaline alisema walimua kufadhili mradi wa usafi wa mazingira baada ya kuona jamii ina muamko mdogo katika matumizi ya vyoo bora.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitatu mabadiliko yameonekana kupitia vijana waliopata ujuzi wa kujenga vyoo wameisaidia jamii yao kujenga kwa gharama nafuu .

Ofisa Afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Christopher Mathias, alisema kuanzia mwaka 2018 hadi 2021 jumla ya vyoo 234 vimejingwa kwenye Kata za Maendeleo, Igoma na Tembela.

## Mapendekezo Bonde la Uyole kuwa manispaa yapitiwa upya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesema wanaangalia upya mapendekezo ya kulifanya Bonde ya Uyole kuwa Manispaa kutokana na jiografia na vigezo vingine kufanyiwa kazi haraka.

Mkakati wa kuigawa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuwa Manispaa mbili ulianza mwaka jana baada ya Hayati Dk. John Magufuli wakati wa kampeni zake, aliwaahidi wananchi wa Mbeya kuwa lazima Jiji la Mbeya ligawanywe ili kuboresha na kusogeza huduma kwa wananchi waishio pembezoni.

Chalamila alisema baada ya mchakato kuanza vikao mbalimbali vimekaa kwa ajili ya majadiliano kupitia baraza la Madiwani,Watendaji wa kata, vijiji, viongozi wa vyama vya siasa na machifu kutoa mapendekezo yao ambao wote walibariki Halmashauri ya Jiji la Mbeya ligawanywe na kuwa na Manispaa mbili.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na wananchi wa Kata ya Igawilo, Chalamila alisema Manispaa zilizopendekezwa ni Manispaa ya Jiji la Mbeya na Manispaa ya Uyole, ambazo zote zimegawanywa kwa kutumia Kata kwa mujibu wa ramani iliyochorwa na wataalam wa mipango Miji.

"Hatujafikia maamuzi ya mwisho kuhusu kuzigawa hizi manispaa kwa sababu bado mapendekezo yanaendelea kutolewa kuna vitu vya msingi inatupasa tuviangalie cha kwanza ni jiografia ya Bonde la Uyole, miundombinu mengine ambayo itakuwa kiunganishi rahisi ili wananchi wapate huduma kwa wakati kuliko ilivyo sasa ambapo kuna mpanglio mbaya wa makazi ya wananchi," alisema Chalamila.

Aliongeza kuwa tayari viwanja 528 vimepimwa katika Kata ya Iduda na kwamba fidia kwa wananchi itakuwa ni zaidi ya shilingi Bilioni moja na kwamba tayari wameanza kulipa fidia hizo.

Alisema hadi sasa wanadaiwa kiasi cha shilingi milioni 400 ili kumaliza kulipa fidia kwa wananchi na kwamba wiki hii watatoa tangazo ili vianze kuuzwa.

Kwa upande wake, Meya wa Jiji la Mbeya, Dormohamed Issa, alisema madiwani kwa kushirikiana na Mkurugenzi wataendelea kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo inayoendelea kujenga na kuanzishwa ili kuchochea uchumi wa Jiji hilo.

Alisema miongoni mwa miradi wanayoendelea kuisimamia kikamilifu ni pamoja na Ujenzi wa Hospitali teule ya Igawilo ambao unaendelea kujengwa na kuboresha majengo mengine ili huduma za matibabu zitolewe kwenye mazingira mazuri.

Aliwaomba wananchi wa Mbeya, kutoa ushirikiano pindi wanapobaini viashiria vya rushwa katika miradi inayoendelea kutekelezwa maeneo mbalimbali ya Jiji ili hatua stahiki zichukuliwe kwa mujibu wa sheria.



# Makamu wa Pili asisitiza ushirikiano kitaifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema taifa linahitaji kuendeshwa katika misingi ya ushirikiano kati ya viongozi na wananchi ili lijielewe linalokusudia kuelekea katika kuihudumia jamii.

Akizungumza jana na waumini wa Dini ya Kiislamu baada ya kukamilika kwa ibada ya sala ya Ishaa na Tarawehe ndani ya Msikiti wa Mkoroshoni, Chake Chake-Pemba, alisema hivi sasa wananchi wameshaunganishwa pamoja katika mfumo huo.

Alisema mtoto lazima asimamiwe kwa nguvu za mzee wake tabia itakayosaidia kupata nguvu za pamoja katika uchungaji wa malezi yatayochangia kurejesha maadili ya taifa yaliyotetereka kutokana na mchanganyiko wa silka na tamaduni za kigeni.

Aliwakumbusha wazazi na wazee wa Mkorokoshoni ambao yeye binafsi aliwahi kuishi kurejesha mfumo wa zamani wa kuwa na vikundi vya polisi jamii vinavyosaidia kuondoa vitendo viovu ikiwamo wizi, matumizi ya dawa za kulevya pamoja na vitendo vya udhalilishaji.

Hemed aliwaeleza waumini na wananchi hao kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejikita kwa nguvu zake kuwaondolea changamoto zinazowakabili wananchi katika maeneo yao akizitaja kuwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma za majisafi, afya na miundombinu ya mawasiliano ya barabara.

Makamu wa Pili yuko Kisiwani Pemba kuungana na waumini wa dini ya Kiislamu na wananchi katika matukio tofauti ya ibada yanayoendelea kutekelezwa ndani ya mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othaman, akimsalimia na kumfariji, Aziza Said Ali (50), ambaye anasumbuliwa na maradhi anayeishi Welezo Wilaya ya Magharibi A Unguja, akiwa katika ziara ya kichama kuwaangalia wagonjwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais Mwinyi awapa mwongozo makamanda wateule

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka makamanda wapya aliowateua kuwa wakuu wa vikosi maalum vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, waende wakajenge na kurudisha nidhamu katika vikosi hivyo.

Katika hafla hiyo iliyofanyika juzi Ikulu, jijini Zanzibar na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali, Rais Mwinyi alisema, jeshi ni nidhamu na ikikosekana hakuna jeshi.

Alisema nidhamu ilitetereka katika vikosi vya Zanzibar na kuamua kuwachangua makamanda hao ili walete uzoefu wao wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Pia, alisema kuwa aliona haja na sababu ya kuwatumia maofisa wa Jeshi la ulinzi la Tanzania ili kuiweka nidhamu katika vikosi vya SMZ.

Aliwataka kwenda kusimamia rasilimali zilizopo katika vikosi hivyo na taasisi walizopewa dhamana kwa kile alichosema kuwapo ubadhirifu mkubwa, wizi na mambo mengine ambayo hayapaswi kufanywa.

Alisema serikali imegundua wahasibu katika vikosi hivyo wanalipa mishahara ya watu ambao hawapo, wanakata posho za askari, pia wanalipa mpaka watu ambao tayari walishastaafu.

Alisema kwamba yeye mwenyewe amethibitisha hayo na hana nia ya kumuonea mtu, aliwataka wakuu hao wapya wa vikosi vya SMZ kuhakikisha wahasibu hawafanyi vitendo hivyo na kutaka yale mambo yasiyofaa yaishe. Rais Dk. Mwinyi alisema kwamba maduka ya vikosi yalikuwa yakitumika vibaya ambapo wahasibu hao walikuwa wakichukua mishahara ya askari kwa kisingizio cha makato ili ionekane walikuwa wamekopa halafu fedha zilikuwa zinakwenda kuchukuliwa madukani.

Alisema kwamba maduka hayo yanadhamira njema ya kuwasaidia maofisa na askari na isiwe vichochoro vya kupitisha fedha haramu.

Katika suala zima la uzalishaji mali, Rais Dk. Mwinyi alisema wakati wa amani kazi ya vikosi vya ulinzi ni mafunzo na uzalishaji mali na kuvitaka vikosi hivyo vikajipange kupunguza ruzuku inayotoka serikalini.

Alivitaka vikosi kupunguza fedha zinazotoka serikali zinazokwenda kwenye vikosi na awamu ya pili iwe kuondokana na ruzuku kwa kujitegemea na kutoa gawiwo kwa serikali na kwamba vikosi hivyo vina fusra za kuzalisha mali.

Rais Dk. Mwinyi alisema ndani ya vikosi kuna viwanda, kampuni ya ulinzi, mashamba, maeneo yanayofaa kwa utalii pamoja na chelezo na kueleza kwamba ipo haja ya kutumika kibiashara na kutaka kuhudumia meli mbali mbali zikiwamo za Zanzibar na nje ya Zanzibar.

Alivitaka vikosi kuingia kwenye ubia na watu wenye uwezo, mashamba yazalishe hasa ikizingatiwa kuwa uwezo huo upo na kutaka vikosi kuzalisha mali ili serikali ipunguze mzigo wa kubeba vikosi hivyo, huku akisisitiza kupatikana kwa haki kwa askari na maofisa na kupata stahili zao kwa wakati.

Alisema hapendi kufukuza watu wala hana nia ya kutafuta mchawi na kufufua makaburi, lakini pale mtu anapokuwa mbadhirifu, wizi wa mali ya umma wa fedha za serikali hatonyamaza na hilo litaendelea mpaka mambo hayo yakome.

Alisema kwamba ndio kwanza anaanza na nguvu bado hazijaisha na kutoa mfano pale alipoivunja Bodi ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), kutokana na ubadhirifu na kutoa angalizo kwa wengine.

Alishangazwa na Bodi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), kwa kufanya ubadhirifu na kusema kwamba kuanzia Januari hadi Machi, bodi hiyo imefanya vikao zaidi ya sita ndani ya miezi mitatu na fedha zilizotumika ni Sh. milioni 99.7.

# JUMAZA yadai kushawishiwa kuondoa kesi mahakamani

**Na Mwandishi wetu,** ZANZIBAR

JUMUIYA ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA), imesema kuna harakati za kuwashawishi waondoe kesi mahakamani waliyoifungua dhidi ya Bodi ya Udhibiti Vileo Zanzibar, lakini hazitofanikiwa mpaka hukumu itakapotolewa Juni 2, mwaka huu.

JUMAZA ilifungua kesi namba 3 ya mwaka 2021, wakidai Bodi ya Udhibiti Vileo imekiuka na kuvunja sheria namba 9 ya mwaka 2020 kwa madai kutolewa vibali kwa kampuji za kuingiza vileo Zanzibar zaidi ya saba badala ya tatu kinyume na sheria

Akizungumza ofisini kwake Majestiki, Katibu Mtendaji wa Jumuiya hiyo, Shekhe Ali Amour, alidai kuna kiongozi wao mmoja ameitwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Vileo na kuomba JUMAZA iondoe kesi mahakamani na madai yao yamalizwe nje ya mahakama.

Hata hivyo, alisema JUMAZA imefungua kesi baada ya sekretarieti yake kujiridhisha umefanyika uvunjwaji na ukiukaji wa sheria mpya ya vileo ukiendelea kufanywa na Bodi hiyo baada ya sheria kupitishwa Baraza la Wawakilishi na kusainiwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mei 11, mwaka 2020 na kuanza kutumika.

"Tumepokea taarifa toka kwa kiongozi wetu mmoja kuitwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Vileo akitaka JUMAZA iondoe kesi mahakamani na madai yetu yamalizwe nje ya mahakama. Hatujaona hoja zozote za msingi hivi kesi itaendelea mahakamani," alisisitiza Shekhe Amour.

Alisema Bodi hiyo inatakiwa kusimamia sheria iliyopitishwa na chombo halali cha kikatiba cha kutunga sheria (Baraza la Wawakilishi) baada ya mijadala kufanyika ngazi mbalimbali toka ngazi za makatibu wakuu Baraza la Mawaziri kabla ya kusainiwa na Rais wa Zanzibar.

Aidha, alisema Jumuiya ya Maimamu Zanzibar inaendeshwa kitaasisi na maamuzi yote hufanyika kupitia vikao vya uongozi ikiwamo sekretarieti na bodi na kusisitiza JUMUITA haiwezi kufuta kesi kienyeji.

Shekhe Amour, alisema JUMAZA kabla ya kwenda kufungua kesi ilishauriana na wanasheria wake ikajiridhisha kuwab Bodi ya vileo imevunja kifungu cha 33 (1) cha sheria ya vileo baada ya kutoa vibali kwa kampuni za uingizaji vileo nane badala ya tatu kinyume na sheria.

Alisema sheria inasema: "Kibali cha kuagiza kitatolewa kwa waagizaji wasiozidi watatu kwa kuzingatia vigezo kwa muingizaji lazima awe ni mzanzibari, mlipa kodi, awe na ghala na gari ya kusambazia vinywaji," alisema akinukuu kifungu cha 33(1) cha sheria mpya ya vileo namba 9 ya mwaka 2020.

Vile vile, alisema pia Bodi ya vileo imevunja kifungu cha sheria cha 28(k) kinachosema leseni ya kuuza au kuhifadhi vileo ghalani itatolewa kwa baa au litakalokuwa na umbali wa mita 1000 kutoka katika shughuli za huduma za kijamii kama hospitali, shule nyumba za ibada au makazi, lakini bodi imeshindwa kusimamia masharti ya sheria hiyo.

# Wakulima korosho watangaziwa neema

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

SERIKALI imesema kuanzia msimu huu wa kilimo, wakulima wa korosho hawatanunua dawa badala yake serikali itawapatia bure, huku wanunuzi wa zao hilo wakichangia gharama hizo.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alitoa kauli hiyo kupitia simu aliyompigia mkuu wa wilaya ya Nanyumbu, Moses Machali, na kuagiza maelekezo yake yawekwe hewani kwa ajili ya kusikilizwa na wajumbe wote waliokuwa kwenye mkutano Mkuu wa 21 wa Chama cha Ushirika Mkoa wa Mtwara (MAMCU).

"Tumebadili mfumo kupitia vikao kadhaa tulivyokaa na viongozi wenu na kwa sasa hamtaenda benki kukopa hela ya kununulia dawa na badala yake jukumu hilo litabebwa na serikali kwa kushirikiana na wanunuzi," alisema Bashe.

Alisema kuwa dawa za kupuliza kwenye korosho zinauzwa kwa fedha isiyozidi shilingi 200 kwa kilo, na kwamba nafasi ya mkulima kuchangia huduma hiyo itakuwa ni baada ya kuuza mazao yake.

Mbali na dawa pia Bashe ameongeza kuwa kwa sasa serikali itanunua mabomba yapatayo 100 ya kunyunyizia dawa na kuzitawanya kwenye AMcoS chache zitazazochaguliwa kwa ajili ya majaribio.

"Leo Mtwara mnafanya uchaguzi, hatutarajii kuona mnaingia kwenye migogoro kwani ninyi ndiyo tunawategemea na mtambue migogoro haihitajiki, kwa kuwa hakuna benki itakayokuwa tayari kuidhamini serikali yenye kupeleka huduma sehemu zenye migogoro"alisema Bashe.

Alisema dawa zitakazogaiwa na serikali zitawekwa nembo maalum kwa ajili ya kuzuia ubadhirifu kutoka kwa watu wasio waaminifu, huku akiwataka wajumbe wa mkutano huo kuachana na siasa za korosho.

"Jielekezeni kwenye kupata mazao bora na achaneni na siasa za korosho, sisi wanasiasa tunalipwa kwa kufanya siasa, lakini ninyi mnalipwa kwa kuwa na mazao yanayouzika sokoni, hivyo muepuke siasa katika hili," alisema.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, aliwataka wakulima wa korosho mkoani humo kujielekeza katika kilimo cha kisasa kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Alisema wakulima wengi wamerithi miti ya mikorosho kutoka kwa wazazi wao, hali inayowafanya wasione umuhimu wa kilimo cha kitaalam, zaidi ya kusubiria msimu wa kuchoma moto mashamba.

Aliongeza kuwa katika kilimo cha kitaalamu mti mmoja wa korosho unapaswa uzalishe kilo kuanzia 100, lakini wakulima wengi hawajui jambo hilo kwa kuwa hawafuati ushauri wa wataalam wa kilimo.

Byakanwa alisema katika utafiti mdogo alioufanya katika Wilaya ya Nanyumbu amebaini kuwa kuna miti milioni nne ya korosho, na kwamba kila mti ungekuwa na uwezo wa kuzalisha walau kilo 20, wilaya hiyo ingekuwa na uwezo wa kuzalisha tani 80,000 kwa mwaka na kuwa wilaya yenye kuzalisha zaidi zao hilo.




Mkuu wa wilaya ya Same mkoa wa Kilimanjaro,Rosemary Senyamule(kushoto) akipokea meza na viti kutoka kwa Meneja wa benki ya NMB kanda ya Kaskazini,Aikansia Muro(wa tatu kulia) kwaajili ya Shule ya Sekondari Kwakoko kuunga mkono sekta ya elimu na kurejesha sehemu ya faida kwa wateja wao,wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo,Anastazia Tutuba na Mwenyekiti wa halmashauri,Yusto Mapande.Jumla ya viti 180 na mabati 192 vyenye thamani ya Sh.25 milioni zilikabidhiwa na benki hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Miradi ya kilimo yageuzwa mahakama

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

JUKWAA Huru la Kilimo (ANSAF), limebainisha vikwazo vinavyoikabili Sekta ya Kilimo nchini, ikiwamo baadhi ya majengo ya miradi ya kilimo kugeuzwa kuwa mahakama.

Owen Nelson, Mtaalamu wa Mnyororo wa Thamani wa asasi hiyo, alibainisha hayo wiki iliyopita jijini Dodoma wakati wa warsha ya kuimarisha uwezo Asasi za Kiraia (AZAKI) zinazotekeleza miradi ya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma (PETS) na uwajibikaji jamii (SAM).

Alisema asasi yao imefuatilia miradi 93 ya Sekta ya Kilimo iliyotekelezwa katika mamlaka 19 za serikali za mitaa kuanzia mwaka 2017 hadi 2020.

Nelson alisema kuwa kati ya miradi hiyo, asilimia 32 imekamilika na kuinufaisha jamii, asilimia 25 iko kwenye utekelezaji, asilimia 31 imekamilika lakini haitumiki na asilimia 12 imetelekezwa.

Alibainisha kuwa wamebaini vikwazo kadhaa katika miradi hiyo ikiwa ni pamoja na kiwango cha chini ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), akisisitiza kuwa tovuti za halmashauri nyingi hazina taarifa za miradi inayotekelezwa na halmashauri husika.

Nelson alikitaja kikwazo kingine kuwa ni kutokutumika kwa miradi iliyokamilika, akigusia kubadilishwa kwa matumizi ya majengo ya miradi ya kilimo. Katika hilo, mtaalamu huyo wa ANSAF aliitolea mfano miradi wa kilimo ya Katerero na Bushasha ambayo majengo yake yanatumika kama ofisi ya kijiji na kata wilayani Bukoba.

Pia, mradi wa kuchakata mpunga na bucha eneo la Mbako umegeuzwa ofisi wilayani Kyela; Soko la Lupa linatumika kama Mahakama ya Wilaya ya Chunya; majengo ya mradi wa Kamwene yamegeuzwa kituo cha mafunzo huko Mlimba; na Kituo cha Upandikizaji cha Makwale kimegeuzwa mahakama huko Kyela.

"Kikwazo kingine tulichokiona kwa Sekta ya Kilimo ni uhaba wa maofisa ugani huku wachache waliopo wakikaimu nafasi za Ofisa Mtendaji wa Kijiji na Ofisa Mtendaji wa Kata.

"Tumeliona hilo katika maeneo ya Kata za Busale (Kyela), Madege (Gairo), Morogoro (Songea) na Karabagaine (Bukoba). Pia, tumebaini kuwapo kwa kikwazo cha wananchi kuiona miradi kama siyo yao, yaani wanasema miradi ya serikali," alibainisha.

Warsha hiyo iliandaliwa na Taasisi ya WAJIBU ikishirikisha asasi na taasisi za serikali zikiwamo HakiElimu, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Bunge, The Foundation for Civil Society (FCS), ANSAF, Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na TACOSODE.

Tekla Mleleu, Ofisa Ufuatiliaji wa Taasisi ya WAJIBU, alisema wanalenga kuimarisha uwezo wa AZAKI zinazofanya miradi ya PETS/SAM kwa kuzipatia taarifa za kifedha za sekta mahususi ili kuboresha ubora na usawa katika utoaji wa huduma ngazi ya halmashauri.

# Bolt ilivyowainua wanawake

**Christina Mwakangale**

IMEELEZWA mfumo wa kidigitali umesaidia kuondoa tofauti za kijinsia na kuwezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika biashara ya usafirishaji.

Esther Chali, ambaye ni dereva kupitia mfumo wa Bolt akizungumza mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam, alisema mfumo huo umempa uhuru na kukuza zaidi kiuchumi.

"Mfumo huu umebadilisha gari langu kuwa rasilimali muhimu ambayo inaniwezesha kujiongezea kipato.

"Naweza kusema mageuzi ya kidigitali duniani yamerahisisha mawasiliano baina ya watu, hivyo imeibua fursa mpya kwa kurahisisha upatikanaji wa huduma na bidhaa mbali mbali," alisema Chali.

Alisema ukuaji wa teknolojia pia umewezesha wanawake kuvuka mipaka na kuanza kushiriki kikamilifu katika shughuli rasmi na zisizo rasmi za kujitafutia kipato.

"Bolt ni mfumo wa kuagiza usafiri kwa njia ya mtandao, unaowaruhusu wasafiri kutumia simu zao za mkononi popote walipo kuomba usafiri wa kuwafikisha popote pale wanapotaka kwenda," alisema na kuongeza:

"Bila kujali jinsia, dereva yeyote mwenye vigezo stahiki katika simu yake ya kiganjani, anajiunga na kuanza kutoa huduma za usafirishaji."

Kadhalika, Esther alibainisha kwamba mfumo huo umepunguza tofauti za kijinsia na kuwawezesha wanawake kujiongezea kipato.

"Umefungua mlango ili tuwe sehemu muhimu ya mfumo mpya wa uchumi unaojulikana kama uchumi wa kugawana, ambao umeibua aina mpya za ajira," alisema Esther..

"Hata siku zile ambazo biashara yangu nyingine inakosa wateja, bado nina uhakika wa kujipatia pesa kutokana na kusafirisha abiria," alisema Chali.

# Wanawake wapewa siri kukua kiuchumi

Na Mary Geofrey

WANAWAKE wametakiwa kujikita kwenye ujasiriamali ili kuendeleza ndoto zao za kukua kiuchumi.

Wito huo umetolewa na Meneja wa taasisi ya Enygma Ventures, Sarah Dusek, wakati akielezea fursa za mfuko wa kuwezesha wanawake kiuchumi katika kulenga masoko ya SADC.

Alisema ni rahisi taasisi za nchi mbalimbi kuwekeza fedha katika makundi ya wanawake wake waliojiajiri ili kuwainua juu kiuchumi kuliko walioajiriwa.

Alisema mradi wao unalenga kuwawezesha wanawake wa nchi za Tanzania na Malawi waliojiajiri na kufikia ndoto za kukuza uchumi.

Alisema taasisi hiyo iliyoanzishwa Oktoba mwaka 2019, kabla ya COVID-19 kuanza kutikisa dunia, mfuko wao uliwekeza dola milioni tatu na nusu kwenye biashara 10 Afrika Kusini, Zambia na Eswatini na kuifanya kuwa moja ya wawekezaji hai mwaka 2020.

"Mwaka huu mfuko unatarajia kuwekeza kwa wanawake wengi zaidi na kulenga masoko makubwa ya SADC kama vile Malawi na Tanzania," alisema Sara.

Alisisitiza kuwa walianzisha Enygma kwa sababu ya kutaka kutatua tatizo la usawa katika nyanja za jinsia, rangi na mazingira.

Alisema wamejikita kupanua wigo huo mwaka huu kwa sababu dhamana ya mfuko wao inajumuisha nchi zote 16 za ukanda wa SADC.

"Kipindi hiki tunategemea kuongeza ushiriki kutoka kwenye masoko yetu muhimu kama Tanzania na Malawi ambazo kwa kipindi cha nyuma zimerekodiwa kuwa na nafasi chache za uwekezaji huku wakiwa na fursa za kuvutia," alisema Sarah.

**Mwaka huu mfuko unatarajia kuwekeza kwa wanawake wengi zaidi na kulenga masoko makubwa ya SADC kama vile Malawi na Tanzania.**

# 'Katiba ya sasa inatosha'

Na Augusta Njoji, DODOMA

HALMASHAURI Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, imesema hakuja haja ya kuwa na Katiba Mpya kwa sasa kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 bado inafaa.

Kimesema katiba hiyo imewezesha kufanyika kwa mabadiliko ya uongozi wa juu serikali, Rais Samia Suluhu Hassan, akishika madaraka bila kuwapo na mgogoro wowote baada ya kutokea kwa kifo cha Rais John Magufuli (pichani).



Akizungumza jana na waandishi wa habari mara baada ya kufanyika kikao cha halmashauri kuu hiyo, Mwenyekiti wa CCM mkoani humo, Godwin Mkanwa, alisema:

"Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Dodoma tunaona Katiba hii ya toleo la 1977 bado inafaa sana na hakuna ulazima wa kuichokonoa, hakuna ulazima wa kutafuta Katiba Mpya wakati hii imetupitisha salama."

Mkanwa alisema katika Katiba Pendekezwa, kuna kifungu kinasema kuwa endapo Rais akifariki dunia akiwa madarakani, lazima zipite siku 90 na baada ya hapo uitishwe uchaguzi wa kujaza nafasi hiyo.

"Halmashauri Kuu inaona kama Katiba Pendekezwa ingekuwa ndiyo Katiba inayotumika sasa, isingetutoa salama," alisema.

Zikiwa zimebaki siku nne kabla ya kufanyika Mkutano Mkuu wa CCM wa kumpitisha Rais Samia kuwa Mwenyekiti wa chama hicho, halmashauri kuu hiyo ya Dodoma imewaomba wajumbe wa kumpitisha kwa asilimia 100 kutokana na uwezo alionao.

Mkutano huo maalum unatarajiwa kufanyika Aprili 30 mwaka huu jijini Dodoma.

Mkanwa aliwaomba wajumbe kumchagua kwa kishindo ili kumpa nguvu ya kutekeleza majukumu yake.

"Kama ambavyo tumemsikia kwa siku hizi 37 tangu awe Rais wetu, ameonyesha mwelekeo ambao kila mtanzania amekubali, tumchagüe kwa asilimia 100 ili sasa tumpe nguvu ya kutekeleza majukumu yake ipasavyo," alisema.

Vilevile, alisema halmashauri kuu hiyo imetoa azimio la kumpongeza Rais Samia na kumpa pole ya kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. Magufuli.




Sehemu ya barabara ya Malinyi katika kijiji cha Misegese eneo la Mwembeni mkoa wa Morogoro, ikiwa imetengenezewa tuta ili kuzuia maji kupita juu ya barabara hiyo iliyoharibika kutokana na mafuriko ya mto Furua, huku kazi nyingine za ukarabati wa barabara hiyo zikiendelea. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Waliokopa fedha h'shauri wapewa siku 14 kurejesha

Na Shaban Njia, KAHAMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, Anderson Msumba, ametoa siku 14 kwa vikundi vya ujasirimali 304 vya vijana na wanawake kurejesha mikopo yao inayofikia Sh. milioni 622 walizokopeshwa na wakishindwa kulipa kwa kipindi hicho watawafikishwa katika vyombo vya sheria.

Aidha, aliwataka madiwani kuvikumbusha vikundi hivyo vilivyopo kwenye kata zao kurejesha mikopo hiyo Ili fedha hizo zitumike kukopesha wengine na kwamba lengo la utoaji wa mikopo hiyo ni kuinua mtaji wa kila mwanachama kupitia vikundi.

Msumba alitoa agizo hilo jana katika kikao cha kawaida cha baraza la madiwani cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2020/2021 wakati akitoa taarifa ya ukopeshaji wa vikundi vya ujasirimali vijana, kinamama na watu wenye ulemavu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 mpaka sasa.

Alisema kuwa tangu walipoanza kutoa mikopo isiyokuwa na riba kwa vikundi vya ujasirimali mwaka 2016, wameshatoa Sh. bilioni 2.6 kati ya kiasi hicho Sh. bilioni 1.12 zimeshareshwa na kiasi cha Sh. milioni 622.3 bado hakijareshwa.

Aidha, Msumba aliwataka watendaji wa kata kushirikisha kamati za maendeleo ya kata (ODC) katika ufuatiliaji wa fedha hizo za mikopo na kuhakikisha zinarejeshwa kwa muda huo ili kuvipatia nafasi vikundi vingine kukopa na kukuza mitaji yao.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Robert Kwela, alisema mwaka wa fedha 2020/2021 wametoa kiasi cha Sh. bilioni 1.5 kati ya fedha hizo kiasi cha Sh. milioni 916 mikopo hiyo ipo ndani ya muda na kuongeza kuwa kushindwa kurejesha mikopo kwa wakati kunakwamisha wengine wasipate.

Alisema vikundi 304 vimekopeshwa na havijarejesha mikopo mpaka sasa.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alisema kuwa mikopo hiyo kwa vijana wengi haiwasaidia kwa sababu wanaichukua na kuielekeza kwenye michezo ya kamari na kushindwa kulipa.

## HABARI MICHEZO



# KOEMAN: NITABAKI BARCELONA MSIMU UJAO

**BARCELONA,** Hispania

RONALD Koeman anatarajia atabakia kwenye nafasi yake ya ukocha hapo Barcelona kwa msimu ujao, wakati timu yake ikipambana kuliwania taji la La-Liga msimu huu.

Raia huyo wa Uholanzi aliletwa hapo kwa mkataba wa miaka miwili kuchukua nafasi ya Quique Setien hapo Agosti, mwaka jana.

Kumekuwa na uvumi kwamba, Rais Joan Laporta anaweza kufikiria kubadilisha kocha msimu ujao, lakini Koeman mwenyewe hana wasiwasi, huku akiwa tayari ameshinda Kombe la Copa del Rey.

Barcelona kwa sasa ipo kwenye mbio za farasi watatu pamoja na Real Madrid na Atletico Madrid kwenye kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu.

Na Koeman amezungumzia uvumi kuhusu hatima yake hapo Katalunya na kusema kuwa anaungwa mkono na Laporta.

"Rais ameonyesha sapoti yake kwangu na ananiamini tangu siku ya kwanza, hadi pale atakaposema vingine, na naamini ana nisapoti," alisema akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa jana Jumapili dhidi ya Villarreal.



# Klopp apoteza matumaini kufuzu Uefa

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp ametoa onyo kwa wachezaji wake wa Liverpool baada ya matumaini yao ya kumaliza kwenye nne bora kufifia, wakati wakitoka sare na Newcastle United, juzi Jumamosi.

Klopp alisema: "Tunajifunza, au hatutaki kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya" msimu ujao.

Wekundu hao walipiga mashuti 22 kwenye lango la wapinzani wao na kufunga bao moja pale katika dimba la Anfield - likifungwa na Mohamed Salah.

Lakini wakajikuta kwenye wakati mgumu baada ya VAR kuwazawadiwa Newcastle bao la kusawazisha dakika ya 92 kupitia kwa Callum Wilson.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Klopp aliiambia BT Sport: "Sidhani kama unaweza kutengeneza nafasi nyingi kama tulivyofanya na tukashindwa kumaliza mchezo.

"Tulifunga bao zuri, lakini halikumaliza mchezo, na hatukucheza vya kutosha. Tulicheza pasi chache na tukashindwa kabisa kumaliza mchezo kwa kufunga mabao zaidi.

"Tuliwaacha watengeneza mashambulizi, na matokeo yake wakapata bao dakika ya mwisho kabisa, kwa hakika hili sio jambo zuri kwetu.

"Kwanini imetokea hivyo, sijui. Lakini lazima tukubali kwamba, tunajifunza au hatutaki kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao."

"Tuna mechi nyingine tano, tutaona tunaweza kufanya nini kwa wakati huo, na tunatakiwa kucheza dhidi ya Manchester United."

# Zidane hana hofu Madrid kupoteza pointi

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane ameonyesha kutulia na kutokuwa na wasiwasi licha ya Real Madrid kushindwa kupata pointi tatu baada ya kulazimishwa suluhu na Real Betis, juzi Jumamosi.

Madrid walionekana wangepaa kileleni mwa msimamo wa LaLiga angalau hadi jana Jumapili kama wangeshinda pale Valdebebas, lakini wakajikuta wakiambulia pointi moja.

Betis walikuwa na nafasi nzuri zaidi kipindi cha pili kwenye mchezo huo, wakati Guido Rodriguez na Borja Iglesias walipokosa nafasi za wazi za kufunga mabao.

Madrid walipiga mashuti matano tu kwenye lango la wapinzani wao, huku Betis wakionekana kukamia zaidi mchezo huo.

Wakiwa wanakabiliwa na mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Chelsea kesho Jumanne, Madrid hawakuwa kwenye kiwango cha kuvutia na kama jana Jumapili Atletico waliwafunga Athletic Bilbao watawapita kwa pointi tano kileleni.

Lakini Zidane alibainisha baada ya mchezo huo kuwa hakuna haja na kuwa na presha, kwani LaLiga bado ina mechi nyingi.

"Tunapoteza pointi, kitu ambacho hatukipendi, lakini LaLiga bado ina mechi nyingi kabla ya kufikia mwisho," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Timu nyingine zote zinatakiwa kucheza vizuri na tutaona mwisho wa siku. Kwa sasa akili yetu ni mchezo wa Jumanne.

"Kiulinzi tulikuwa vizuri, lakini hatukuwa na kasi ya kusukumiza mashambulizi mbele na tulikosa vitu vingi.

"Hatukuwa kwenye ubora wetu uwanjani, naamini kuna jambo la kujifunza na mambo yatakwenda sawa tu."



# Garcia, Barcelona wafikia pazuri

**BARCELONA,** Hispania

MAZUNGUMZO kati ya mlinzi wa Manchester City, Eric Garcia na Barcelona yamefikia katika hatua nzuri, kwa mujibu wa Mundo Deportivo.

Nyota huyo aliyekulia katika akademi ya Barcelona, kwa muda mrefu alikuwa akitajwa kutaka kurejea katika klabu yake hiyo ya zamani.


Kwa mujibu wa ripoti, majadiliano ya mwisho yamefanyika Alhamisi, kukiwa na ishara ya kufikia hatua nzuri ya mazungumzo.

Pande zote zinaamini kuwa dili hilo litakamilika na Garcia ana uhakika wa kuvaa jezi za Barcelona msimu ujao.

Kulikuwa na kupanda na kushuka kwenye biashara ya Barcelona kumnasa Garcia, ambaye alifanya makubaliano na klabu yake hiyo ya zamani, lakini mipango yote haikukaa sawa, suala la changamoto za kiuchumi likihusika na masuala mengine ya kiuongozi.

Lakini baada ya Joan Laporta kushika hatamu kama rais wa Barcelona, amezungumza na wakala wa Garcia, Ivan de la Pena na ameeleza kuwa kwa sababu ya changamoto walizokuwa wanapitia waliona dili hilo lingefikia hatua ambayo ingeonekana kutokuwa na manufaa mazuri kwa mchezaji huyo.

Taarifa zinasema Barcelona wameahidi kuuboresha mkataba na malipo kwa mchezaji huyo.






# SALAH AJIWEKEA REKODI LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah ameweka rekodi mpya katika timu ya Liverpool kwa kuwa mchezaji wa kwanza kufikisha mabao 20 katika misimu mitatu tofauti ya Ligi Kuu England.

Salah alifikisha bao la 20 msimu huu katika mchezo wa Liverpool dhidi ya Newcastle United wakati alipofunga dakika ya tatu, mchezo ukimalizika kwa sare ya 1-1, juzi Jumamosi.

Anfield imekuwa ikipongezwa kwa kutoa wachezaji wenye vipaji vya kushambulia kwa miaka kadhaa, kuanzia Robbie Fowler hadi Luis Suarez kupitia Fernando Torres, lakini hakuna anayeweza kufikisha rekodi ya nyota huyo wa sasa.

Salah amekuwa mfano wa uthabiti wa wakati wote pale Merseyside, na viwango vya kushangaza vimedumishwa katika msimu huu wa 2020-21.

Salah alisajiliwa na Liverpool akitokea AS Roma msimu wa kipindi cha majira ya joto mwaka 2017.

Mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea aliendana na soka la Uingereza, akifanikiwa kufunga mabao 44 kwenye mashindano yote kwenye msimu wake wa kwanza.

Kati ya hayo, 32 alifunga kwenye Ligi Kuu England, ambayo yalitosha kupata kiatu cha dhahabu kama mfungaji bora.

# *Conte ajisifia kujenga timu ya ushindi*

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte amesema alianzia sifuri kuijenga Juventus katika hali ya kushinda, kitu ambacho pia anakifanya sasa akiwa Inter Milan.


Inter wapo nafasi ya kwanza kwenye msimamo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa tofauti ya pointi 10 na AC Milan iliyopo nafasi ya pili, licha ya kutoka sare mfululizo dhidi ya Napoli na Spezia.

Conte alirejesha njaa ya ushindi wa mataji akiwa na Juventus, na sasa anasaka kumaliza ukame wa mataji pale Inter Milan baada ya miaka 11.

Kuhusu hatima yake Inter, Conte amesema hakuna mtu anafahamu kuhusu kesho, isipokuwa kuhusu suala la kutengeneza na kuhamasisha hali ya ushindi kwa Inter.

“Kwa suala la kutengeneza saikolojia ya ushindi, tulikuwa tunaanzia sifuri pale Juventus, hivyo hii siyo mara ya kwanza,” alisema akinukuliwa na Sky Sport Italia.

“Ukiachana na mawazo, kitu ambacho kocha anakihitaji zaidi ni kutafuta wachezaji ambao wanajitoa kujipa changamoto na kufanya kitu kipya.”



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE HATIHATI KUIVAA MAN CITY

●●● Kocha wake Pochettino amesema itakuwa pigo endapo straika huyo ataukosa mchezo...

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe hayupo kwenye hatari ya kuukosa mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City Jumatano, licha ya kuumia Jumamosi.

Mbappe alifunga mabao mawili wakati PSG ikishinda magoli 3-1 dhidi ya Metz kwenye mchezo wa Ligi Kuu Ufaransa na kuwapandisha kileleni mwa msimamo, juzi Jumamosi.

Mabao hayo yalimfanya Mbappe kufikisha magoli 19 aliyohusika nayo ugenini msimu huu, mengi zaidi kuliko mchezaji yoyote kwenye ligi kubwa tano za Ulaya, akiwazidi Erling Haaland (10) na Robert Lewandowski (tisa).

**Fowadi huyo wa Ufaransa ameendelea kuwa moto, kwani amefikisha mabao tisa katika mechi saba za ligi zilizopita.**

Kulikuwa na shaka kuhusu hali ya Mbappe ambaye alionekana kuumia goti na hivyo nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 kulazimika kutolewa nje.

Lakini Kocha, Mauricio Pochettino hana hofu kuhusu straika wake huyo kwamba anaweza kukosa mchezo dhidi ya City.

"Ni pigo kwa kikosi," alisema Pochettino akiiambia Canal Plus.

"Sidhani kama ni kwa kiasi kikubwa, tuna matumaini hajaumia sana.

"Sifikirii kama anaweza kuwa hatarini kuukosa mchezo wa Jumatano. Kwa sasa ni pigo tu la kawaida. Haitupi sisi presha kubwa kwamba anaweza kuukosa mchezo wa City.

"Kylian alitulia wakati akitolewa nje, ingawa alionekana kuwa na maumivu makali."

## ZISIKUPITE

### UNITED, ARSENAL VITANI

MANCHESTET United na Arsenal ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia fowadi wa Borussia Monchengladbach na Ufaransa, Alassane Plea ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Mail)***

### SHAW MAMBO MAZURI

MLINZI wa kushoto wa Manchester United na England, Luke Shaw mwenye umri wa miaka 25, anatarajia kusaini mkataba mpya baada ya kuwa kwenye kiwango cha kuvutia msimu huu. ***(Star)***

### SOLSKJAER, CAVANI WATETA

STRAIKA wa Uruguay, Edinson Cavani amefanya mazungumzo na kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer kuhusu kuongeza mkataba wa mwaka mmoja - lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 anakaribia kuondoka hapo Old Trafford. ***(Mirror)***

### INTER YAMGANDA AGUERO

INTER bado imebakia kwenye mawindo ya kumsajili straika wa Manchester City na Argentina, Sergio Aguero lakini Barcelona bado wana nafasi kubwa ya kuipata saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32. ***(Tuttosport, via Sun)***

### TAGLIAFICO SOKONI

AJAX wapo tayari kumuuza mlinzi wao, Nicolas Tagliafico mwenye umri wa miaka 28, kwa pauni milioni 13, huku Leeds United, Manchester City na Inter Milan zote zikimwania. ***(Mail)***

### UNITED KUUZWA

WAMILIKI wa Manchester United, Glazers wamepanga bei ya kuiuza klabu hiyo ya pauni bilioni nne, baada ya mashabiki kuandamana nje ya uwanja wa Old Trafford siku ya Jumamosi. ***(Mirror)***

### BILIONEA AITAKA ARSENAL

MMLIKI wa Kampuni ya Spotify, bilionea Daniel Ek anajiandaa kununua hisa Arsenal, baada ya kuchapisha nia yake hiyo Ijumaa kwenye ukurasa wake wa Twitter. ***(Telegraph - subscription required)***

### HEATON ANUKIA UNITED

MANCHESTER United wanaangalia uwezekano wa kumsajili golikipa wa Aston Villa, Tom Heaton mwenye umri wa miaka 35. ***(Sun)***

### PSG: HATUNA HARAKA

MKURUGENZI wa michezo wa Paris St-Germain, Leonardo amesema klabu hiyo ya Ufaransa haina haraka katika mkataba mpya wa fowadi wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 29. ***(Goal)***

### HAALAND, LUKAKU WATAJWA

CHELSEA inataka kumsajili straika mpya kipindi cha majira ya joto kinachokuja, huku fowadi wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland, 20, na Romelu Lukaku (27), wa Inter Milan, wakiongoza kwenye orodha yao. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

## Gulioni yafunguka sababu kuvurunda

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Gulioni FC inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja imesema kusuasua kwa timu yao kumetokana na 'ugeni' walionao katika ligi hiyo ngumu na yenye ushindani ambayo wanashiriki kwa mara ya kwanza msimu huu, imefahamika.

Makamu Mwenyekiti wa Gulioni, Mussa Issa aliliambia gazeti hili timu yake imepanda daraja msimu uliopita hivyo wachezaji wao bado hawajapata uzoefu kwa kukabiliana na ushindani uliopo kwenye ligi hiyo kama walivyo wapinzani wao.

Issa alisema kukosa uzoefu na kutojiamini kwa wachezaji wake wanapokutana na timu pinzani kunapelekea kupoteza mechi wanazocheza lakini wameshaanza kufanyia kazi mapungufu hao waliyoyabaini.

Alisema kocha wa timu yao hana tatizo kama baadhi ya mashabiki wanavyodhani na kuweka wazi wachezaji wao ndio wanakosa umakini huku pia wakicheza na hofu.

Alisema bado hawajakata tamaa na hivi sasa wanazielekeza nguvu zao kuhakikisha wanapata ushindi katika michezo yao mitano iliyobakia ya kumaliza msimu huu ili wasishuke daraja.

## Singida yajipanga kuwanoa makocha

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

WANAFUNZI mbalimbali kutoka katika Shule za Msingi na Sekondari wanatarajiwa kushiriki mafunzo ya awali ya michezo ya riadha, wavu na mpira wa mikono yatakayofanyika kwenye viwanja vya michezo vya Mwenge mkoani hapa.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwaongezea uwezo wa kufundisha wanafunzi katika shule mbalimbali wanazotoka.

Ofisa Maendeleo wa Michezo wa Mkoa wa Singida, Henry Kapera alisema mafunzo hayo yatasaidia kuleta tija watakaposhiriki katika mashindano ya michezo ya Umiseta na Umitashimuta.

Aliongeza mafunzo hayo yanafanyika ikiwa ni katika mkakati wa kuhakikisha mkoa unatoa wanamichezo wazuri watakaokwenda kupeperusha vyema bendera ya Singida kwenye mashindano ya Umiseta na Umitashimuta.

Naye Ofisa Maendeleo ya Michezo wa Halmashauri za Wilaya ya Ikungi, Abubakari Kisuda alitumia wasaa huo kutoa wito kwa wadau wa michezo wa nje na ndani ya mkoa wa Singida kuwaunga mkono katika kuendeleza sekta ya michezo mkoani hapa.

# PRISONS YAITANGAZIA VITA YANGA KUELEKEA FA CUP

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shabani Kazumba amesema wanahitaji kumaliza mechi ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Yanga dakika 45 za kipindi cha kwanza ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

**Tanzania Prisons inatarajia kuikaribisha Yanga katika mchezo wa hatua ya 16 Bora ya Kombe la FA utakaochezwa Aprili 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela ulioko Sumbawanga mkoani Rukwa.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kazumba alisena wamejipanga vizuri kuhakikisha wanawaondoa Yanga katika michuano hiyo kwa kuwafunga mapema.

Kazumba alisema wamedhamiria kuendeleza 'ubabe' dhidi ya timu za Kariakoo (Simba na Yanga), kwa kupata matokeo chanya kila wanapokutana.

"Hatutaki kupata kazi ya kwenda nao hadi dakika 90 au kupigiana penalti, tunahitaji kumaliza mchezo huo ndani ya dakika 45 za kipindi cha kwanza, tunapokwenda mapumziko tuwe tunaongoza kwa mabao 2-0 au zaidi," alisema Kazumba.

Alisema wanahitaji kucheza robo na nusu fainali ya michuano hiyo na wanaimani ya kufanya vizuri kutokana na utulivu uliopo ndani ya benchi lao la ufundi ambalo limedumu kwa muda mrefu na kuwatengenezea wachezaji inayofanana tofauti na wapinzani wao ambao wamebadilisha makocha mara tatu msimu huu.

"Yanga wana kikosi kizuri na wachezaji wake pia kama ilivyo kwetu, ila tofauti ya wenzetu ni kuondoka kwa makocha wao, ukizingatia huyo aliyekuja naye amekuja na mipango yake ambayo kwetu hatutawapa nafasi ya kupata mafanikio," alisema Kazumba.

Bingwa wa michuano ya Kombe la FA atapata nafasi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika ambayo huandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).



Muogeleaji mahiri wa hapa nchini, Hilal Hilal akiwa katika moja ya mashindano aliyowahi kushiriki na kuiwakilisha vyema Tanzania. Kwa sasa Hilal yuko Dubai akifanya mazoezi kwa ajili ya kushiriki mashindano ya kusaka tiketi ya kucheza Michezo ya Olimpiki itakayofanyika Julai, mwaka huu nchini Japan. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Kuogelea waiomba serikali kuwabeba*

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Kuogelea Tanzania (TSA), kimeomba msaada kwa Serikali kusaidia gharama za safari ya waogeleaji wawili pamoja na kocha kwenda Afrika Kusini kushiriki mashindano ya kutafuta nafasi ya kufuzu michuano ya Olimpiki itakayofanyika Julai, mwaka huu jijini Tokyo, Japan.

Mashindano ya kutafuta tiketi ya kufuzu kwa ajili ya Olimpiki yamepangwa kufanyika Mei 7 na 8, mwaka huu katika mji wa Stellenbosch na Watanzania Hilal Hilal na Collins Saliboko wamechaguliwa kuiwakilisha Tanzania.

Waogeleaji hao watakuwa chini ya kocha Alexander Mwaipasi na gharama za safari yao ni Sh. milioni 10 wakati Shirikisho la Mchezo huo la Afrika (Cana), limethibitisha kugharamia chakula na malazi kwa wanamichezo wote watakaofika Afrika Kusini.

Katibu Mkuu wa TSA, Inviolatha Itatiro alisema chama hicho kwa sasa hakina fedha kwa ajili ya kununua tiketi ndio maana wameliwasilisha ombi hilo kwa serikali.

Itatiro alisema wamefanya hivyo kwa sababu wamekuwa na vikao kadhaa na serikali kupitia kwa Baraza la Michezo Tanzania (BMT) na Mkurugenzi wa Maendelea ya Michezo Nchini, Yusuph Singo vyenye lengo la kuongeza nafasi ya kufuzu kwa wanamichezo wa Tanzania katika mashindano ya Olimpiki.


"Vikao hivyo vilikuwa pia vinashirikisha vyama vingine kama ngumi za ridhaa, judo na riadha. Pia TOC nayo ilishiriki katika vikao hivyo na serikali imekuwa ikiahidi kusaidia vyama ili vishiriki katika mashindano ya kufuzu," alisema Itatiro.

Aliongeza waogeleaji hao wanatakiwa kuripoti Afrika Kusini ifikapo Mei Mosi na wakifika huko wataanza kushiriki mafunzo maalumu ambayo yatayoendeshwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ufundi ya Shirikisho la mchezo wa kuogelea duniani (Fina), Graham Hill.

# Michezo

Jumatatu Aprili 26, 2021

Nipashe

Mbappe hatihati kuivaa Man City UKURASA 22



Golikipa wa Gwambina FC, Mohamed Makaka (kulia), akiwania mpira dhidi ya kiungo wa Simba, Clatous Chama katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Gwambina ulioko Misungwi jijini Mwanza juzi. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: SIMBA**

# Waziri: Klabu ziige uwekezaji Simba

## ●●● Ni wa Bilionea Mo Dewji uliochagiza mafanikio michuano ya kimataifa...

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, ameipongeza Tume ya Ushindani (FCC) na Klabu ya Simba kwa kumaliza mgogoro wa kiuwekezaji, akizitaka klabu zingine za soka nchini kuiga mfano huo wa uwekezaji ili kuleta maendeleo ya mchezo huo nchini.

**Bashungwa alitoa pongezi hizo juzi alipotembelea Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Michezo cha Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ulioko Kigamboni, jijini Dar es Salaam.**

"Ninazikaribisha klabu zingine kushirikiana na serikali ili kuendana na Dira ya Serikali na maelekezo ya Rais wetu, Samia Suluhu Hassan, ya kutaka sekta hii kutoa ajira kubwa kwa vijana na kuchangia kwenye pato la nchi," alisema.

Bashungwa (pichani) pia alitumia nafasi hiyo kuipongeza Simba kwa kufika hatua ya robo fainali katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku akiwataka Watanzania kuonyesha uzalendo kwa kuiunga mkono klabu hiyo inayoitangaza Tanzania kimataifa na kupitia kauli mbiu yao ya Visit Tanzania (Tembelea Tanzania) katika jezi zao.



Katika ziara yake hiyo, waziri huyo alikagua mradi huo unaofadhiliwa na Shirikisho la Soka la Duniani (FIFA), akishuhudia shughuli za ujenzi zikiendelea na kujiridhisha na kutoa rai kwa uongozi kufanikisha ujenzi wa viwanja vinne kufikia mwishoni mwa mwaka huu.

Rais wa TFF, Wallace Karia, alibainisha huduma za kimichezo zitakazokuwa zinapatikana kwenye mradi huo unaotekelezwa Dar es Salaam na Tanga, kuwa ni mpira wa miguu kwa viwanja vya nyasi bandia na za kawaida, hoteli ya hadhi ya nyota tatu, hosteli kwa wakufunzi wanamichezo, viwanja vya mpira wa wavu na pete na mabwawa ya kuogelea.

# Yanga: Tutamaliza VPL kwa heshima

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi amesema hana hofu na mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara zilizopo sasa na kuongeza 'hesabu' zitakamilika vyema katika mechi ya mwisho ya kumaliza msimu wa 2020/21 na si vinginevyo.

Nabi alisema timu kuongoza au kutoongoza kwa sasa si muhimu sana, kama ambavyo itakuwa hivyo siku ya mwisho ya kumaliza ligi.

"Kwa sasa kila mmoja anajipanga kupata ushindi ili kujiimarisha, huwezi kujua nini kitatokea katika mechi zilizobakia, hakuna ambaye ana uhakika na kile ambacho anakitaka, tutaendelea kujipanga kutafuta matokeo mazuri," alisema Nabi.

Naye Kocha wa viungo, Jawadi Sabri alisema anaamini Yanga itakuwa na kikosi imara ambacho kitavuna matokeo bora kwenye mechi zilizosalia za ligi hiyo inayoelekea ukingoni.

"Ninaamini tutakuwa na neema katika klabu hii, tumekuja kufanya kazi na matunda yataonekana, tuendelee kujituma ili kufikia malengo," alisema Sabri ambaye alitua nchini kuchukua mikoba iliyoachwa na Mghana, Edem Mortotsi ambaye alitimuliwa sambamba na Cedric Kaze.

Sabri alisema amewaandalia wachezaji wa Yanga programu mbalimbali ambazo zitawaimarisha na kuwarejesha kwenye ubora wao ambao utasaidia kuwapa changamoto wapinzani watakaokutana nao.

"Wameshaanza kubadilika, tutarajie kuwaona wakiwa tofauti na kwenye viwango bora, ninaamini tutapata kile tunachokihitaji, hakuna timu itakayopata wakati mwepesi tukikutana nayo," Sabri alisema.

Baada ya mechi ya jana usiku dhidi ya Azam FC, kikosi cha Yanga kitajiandaa na safari ya kuelekea Sumbawanga kuwafuata Tanzania Prisons kwa ajili ya mchezo wa hatua ya 16 Bora ya mashindano ya Kombe la FA utakaochezwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela.

Simba ndio mabingwa watetezi wa michuano ya Kombe la FA na Ligi Kuu Tanzania Bara.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >